# Nipashe

Jumatano Novemba 4, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580389

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710


**VIKUMBO** uchaguzi wenyeviti, mameya halmashauri vyaanza

UKURASA 4



UKURASA 3

**NCCR- MAGEUZI** yasema uchaguzi mkuu ulivurugwa




UKURASA 11

# MSEKWA: Bunge lijalo litakuwa hivi



UKURASA 2



Aliyekuwa Spika wa Bunge, Job Ndugai (kushoto), akipokea fomu ya kuomba kuteuliwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM), kugombea tena nafasi hiyo, kutoka kwa Katibu Msaidizi Mkuu Idara ya Organaizesheni Makao Makuu ya chama hicho, Solomon Itunda, jijini Dodoma jana.
**PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mbowe aachiwa, Zitto mbaroni madai kuchochea maandamano

UKURASA 2

## YALIYOMO


**UKURASA WA 4**

**TRA YAKAMATA SHEHENA YA SUKARI**
MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imekamata shehena ya bidhaa mbalimbali, ikiwamo sukari katika mpaka wa...

**UKURASA WA 4**

**MGOMBEA WA UBUNGE AACHIWA KWA DHAMANA**
MAHAKAMA ya Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera imewaachia kwa dhamana ya Sh. milioni tano kila mmoja washtakiwa sita akiwamo aliyekuwa mgombea wa...

**UKURASA WA 5**

**WANUSURIKA KIFO BAADA YA GARI KUBOMOA NYUMBA**
WATU watatu, wakiwamo mume na mke ambao ni wamiliki wa duka la dawa za binadamu...


## Ndugai, Dk. Tulia kutetea nafasi zao

UKURASA 3

**MICHEZO** POLISI TANZANIA WAZITAKA TATU ZA MBEYA CITY KESHO UK. 23

MAONI, KATUNI UK. 6

# Zitto akamatwa, Mbowe aachiwa

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, limemkamata na baadaye kumwachia kwa dhamana Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, kwa tuhuma za kuhamasisha maandamano kupinga matokeo ya uchaguzi mkuu uliofanyika wiki iliyopita.

Mbali na Zitto, viongozi wengine wa vyama vya upinzani walioachiwa jana baada ya kushikiliwa na jeshi kwa tuhuma hizo ni pamoja na Freeman Mbowe, Godbless Lema na Boniface Jacob.

Kamanda wa Polisi wa kanda hiyo, Lazaro Mambosasa, aliliambia Nipashe jana jioni kuwa walimkamata na kumshikilia Zitto kwa tuhuma za kufanya kosa hilo.

"Ni kweli tunamshikilia Zitto kwa sababu ambazo tumeshazieleza awali kwamba viongozi wamekusanyana Dar es Salaam kwa ajili ya kuingia barabarani, sababu ni hiyo hiyo," alisema.

Hata hivyo, jeshi hilo lilimwachia kiongozi huyo wa upinzani na wenzake kadhaa ambao inadaiwa alikamatwa wakati wanakwenda kuwajulia hali mahabusu ya polisi walikokuwa wamehifadhiwa.

Jumamosi iliyopita, Zitto, akiwa katika mkutano uliohusisha chama chake na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), alisema hawakubaliani na matokeo ya uchaguzi huo uliokipa ushindi mkubwa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Zitto alisema hayo baada ya Mwenyekiti wa Taifa CHADEMA, Mbowe, kusoma tamko la pamoja la vyama hivyo lililotokana na vikao vyao vilivyofanyika kwa siku mbili jijini.

"Mahali tulipofikishwa ni lazima ama tukubaliane na ukweli au uongo, kukubaliana na haki au ukandamizaji ila uamuzi ni kukubaliana na ukweli na kukataa uongo, kukubaliana na haki na kupinga ukandamizaji," alisema Zitto.

Alisema hilo siyo jambo kwa ajili ya CCM au upinzani bali ni kuhusiana na muhstakabali wa Tanzania.

"Tukiendelea namna hii na kukubaliana na kilichotokea maana yake ni kwamba tunairudisha nchi katika mfumo wa chama kimoja, kama viongozi hatukubaliani na hali hii tupo tayari kuongoza harakati za kudai haki, kutetea demokarasia na kuilinda nchi.

"Salamu kutoka kwa Maalim Seif ndiyo hizo alizosoma Mbowe na haya ni maandamano yasiyo na kikomo ya nchi nzima Tanzania bara na Zanzabar," alisema.



Aliyekuwa Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson (kushoto), akipokea fomu ya kuomba kuteuliwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM), kugombea nafasi hiyo tena, kutoka kwa Katibu Msaidizi Mkuu wa Idara ya Oganaizesheni ya chama hicho, Solomon Itunda, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Msekwa: Bunge lijalo litakuwa la namna hii

**Na Beatrice Shayo**

SPIKA mstaafu wa Bunge la Tanzania, Pius Msekwa, amesema Bunge lijalo litakuwa na mageuzi makubwa ya kukosekana kwa mambo manne yaliyokuwa yamezoeleka kwenye taratibu za uendeshaji wake.

Msekwa amesema mabadiliko hayo ni zao la mageuzi makubwa yaliyoshuhudiwa katika matokeo ya kura, yanayozaa mabadiliko makubwa ya sura ya upinzani bungeni, ikiwamo kushindwa kuunda kisheria Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Katika mazungumzo na Nipashe jana, Msekwa aliyekuwa Spika wa Bunge hilo (Aprili 1994 hadi Novemba 2005), alisema kutokana na anguko kubwa la upinzani katika uchaguzi wa mwaka huu, iko wazi kwamba Bunge la 12 halitakuwa na Kambi Rasmi ya Upinzani.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba wabunge wa upinzani watakaokwenda bungeni, hawatafikia asilimia 12.5 ya wabunge wote inayohitajika kikanuni ili kuunda kambi hiyo.

"Kambi Rasmi ya Upinzani maana yake ni kitengo kinachoundwa na wapinzani ili kupambana na mawaziri wa serikali bungeni, ndiyo maana kila wizara inakuwa na msemaji wa wapinzani, wanaitwa mawaziri Kivuli.

"Kwa matokeo haya (ya uchaguzi), maana yake hapatakuwa na mawaziri kivuli, hata mmoja watakuwapo kama wabunge mmoja mmoja, yaani Kambi Rasmi ya Upinzani yenye Kiongozi wa Kambi na mawaziri kivuli haitakuwapo bungeni," alifafanua.

Msekwa alisema jambo hilo linatokea kwa mara ya kwanza tangu nchi iingie kwenye mfumo wa vyama vingi, akisema miaka ya nyuma nchi ilikuwa na wabunge wa kutosha kuunda baraza la mawaziri kivuli.

"Safari hii ni mara ya kwanza wamekosa, wananchi wamewakosesha, haijawahi kutokea tangu kuanza mfumo wa vyama vingi kukosekana Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni," alikumbusha.

Hata hivyo, Msekwa alisema kukosekana kwa kambi hiyo hakutakuwa na tatizo kwa kuwa anaamini wabunge wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) watajitokeza kuwakosoa mawaziri.

Msekwa alisema anaamini lazima mawaziri watakumbana na ukosoaji kwa kuwa maswali yatawasilishwa kama ilivyo kawaida.

"Watu walikuwa wanafuatilia wakati wa bajeti wabunge wa upinzani wanakataa kila kitu, lakini wa CCM wanakosoa na kueleza hapa kuna upungufu fulani... wanashauri cha kufanya, hiyo ndiyo tija yenyewe na tija siyo kupinga, ni kuboresha mapendekezo ya serikali badala ya kupinga kila kitu," alisema.

Msekwa alisema Bunge kukosa mawaziri kivuli kutaathiri hotuba za upinzani, lakini anaamini zitawasilishwa kwa mbinu nyingine ambayo ni kupitia michango ya wabunge wachache wa upinzani.

"Wale wanane (huenda idadi ikaongezeka) watakaokuwapo bungeni, watatoa hotuba, ambacho hakitakuwapo ni mawaziri kivuli, watambue kuna tofauti kubwa ya kupinga na kuboresha. Kupinga siyo tija bali kuboresha kunaleta tija," Msekwa alionya.

"Kila mbunge ana wajibu wa kutoa hotuba kwa muda aliopangiwa na spika anapokuwa bungeni. Kwani upande wa serikali ni mawaziri pekee yao wanaotoa hotuba?

"Kila mbunge wa CCM anatoa hotuba yake, kila mbunge ana haki ya kupewa nafasi ya kusema bungeni ama hotuba ama kuongea ndiyo maana unapangiwa muda kama ni dakika 15 unaongea vile unavyotaka, ukimaliza hotuba yako unapigiwa kengele ya muda," alisema.

Fursa nyingine ambayo upinzani utaikosa katika Bunge la 12, ni upendeleo wa kikanuni ambazo zinataka Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bunge awe wa kwanza kumuuliza swali Waziri Mkuu wakati wa kipindi cha 'Maswali kwa Waziri Mkuu'.

Kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Toleo la Januari 2016, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni pia anapewa nafasi ya kusimama wakati wowote bungeni na kuchangia hoja na mbunge mwingine yeyote aliyekuwa anazungumza kwa wakati huo hulazimika kusitisha ili kutoa nafasi kwa kiongozi huyo.

**KANUNI ZINASEMAJE?**

Kwa mujibu wa Kanuni ya 14(2), wabunge wote wa upinzani wanaweza kuunda Kambi Rasmi ya Upinzani iwapo idadi yao itakuwa siyo chini ya asilimia 12.5 ya wabunge wote.

Kanuni ya 14(3) inasema chama cha upinzani hakitakuwa na haki ya kuchagua Kiongozi wa Upinzani Bungeni, isipokuwa tu kama kina idadi ya wabunge wasiopungua asilimia 12.5 ya wabunge wote.

"Endapo kutakuwa na vyama vya upinzani zaidi ya kimoja ambavyo kila kimoja kina wabunge asilimia 12.5 au zaidi, basi chama chenye idadi kubwa zaidi ya wabunge kuliko vingine ndicho kitakuwa na haki ya kuchagua Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

"Lakini, ikiwa kutakuwa na vyama viwili au zaidi vyenye idadi sawa ya wabunge ambao ni zaidi ya asilimia 12.5, wabunge wa vyama vinavyohusika watachagua Kiongozi wa Upinzani Bungeni chini ya utaratibu watakaokubaliana wenyewe.

"Chama chenye haki ya kumchagua Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kinaweza pia kuchagua Naibu Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

"Chama kinachounda serikali na chama chenye haki ya kuchagua Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, vitateua wanadhimu wa vyama hivyo bungeni ambao watajulikana kwa jina la Mnadhimu wa Serikali na Mnadhimu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni," inafafanuliwa zaidi katika Kanuni ya 15 na 16.

Katika uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28 mwaka huu, vyama vya upinzani vimefanya vibaya, CHADEMA iliyokuwa na wabunge wengi Bunge la 11 imeshinda ubunge katika jimbo moja, ACT-Wazalendo iliyokuwa na mbunge mmoja Bunge lililopita, ikipata wabunge wanne huku CUF ikiambulia wabunge watatu.

Baada ya mchakato wa uchaguzi huo kukamilika, kinachosubiriwa sasa ni wabunge watokanao na uteuzi wa Rais (nafasi 10) na wale wa viti maalum ambao uteuzi wao hufanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kwa kuzingatia uwiano wa kura ambazo kila chama kimepata kwenye majimbo.




Mkuu wa Idara ya Uenezi na Mahusiano ya Umma wa Chama cha NCCR-Mageuzi Taifa, Edward Simbeye (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu matokeo ya uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, 2020. Kulia ni Kamishna wa Chama hicho, Mkoa wa Dar es Salaam, Mustafa Muro. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# NCCR-Mageuzi yadai uchaguzi ulivurugwa

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha NCCR-Mageuzi kimesema matokeo ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu hayawezi kuhalalisha aliyeshinda na aliyeshindwa kwa kuwa mchakato wake ulivurugika.

Kimedai mchakato wa uchaguzi huo ulikuwa na dosari nyingi kuanzia hatua ya mwanzo hadi mwisho, hivyo matokeo yake hayawezi kuwa halali.

Hata hivyo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kupitia kwa Mkurugenzi wake wa Uchaguzi, Dk. Wilson Mahera, ilisema juzi kuwa uchaguzi umeshakwisha lakini inajua kila mtu anazungumza lake.

Jana, Mkuu wa Idara ya Uenezi na Uhusiano wa NCCR-Mageuzi, Edward Simbeye, katika mkutano wake na waandishi wa habari kuhusu msimamo wa chama chao kuhusu uchaguzi huo, alidai chama chao kilikuwa cha kwanza kuwasiliana na tume kulalamikia mwenendo wa uchaguzi.

Alisema kuwa waliwasiliana na tume kutoa tahadhari juu ya mwenendo usiofaa wa wasimamizi na wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi.

Alisema kuwa mambo yote waliyotahadharisha kwa tume hiyo, ndiyo baadaye yalijitokeza wakati wa uchaguzi na kuibua shutuma kwa tume hiyo kushindwa kuusimamia vizuri uchaguzi huo.

"Tuliyokuwa tunayasema ndiyo yametokea, kituo kama Kawe mgombea wetu wa ubunge hata kura yake haipo, ukienda katika majumuisho jioni alikuwa ana kura sifuri. Kule Vunjo robo tatu ya mawakala hawakuingia katika vituo hadi ilipofika saa sita mchana," alidai.

NCCR-Mageuzi ambayo katika Bunge la 11 ilikuwa na mbunge mmoja, safari hii haijapata hata jimbo moja la kuliwakilisha bungeni.

# Ndugai, Tulia wajitosa kuwania nafasi zao

**Na Waandishi Wetu,** DODOMA

SPIKA wa Bunge la 11, Job Ndugai, amechukua fomu ya kugombea tena uspika wa bunge lijalo, huku akiwaomba Watanzania wamwombee ili Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimteue kutetea nafasi hiyo.

Pia Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, amechukua fomu huku akisema anatarajia kuona wabunge wa Bunge la 12 wanafanya kazi ya kuwawakilisha wananchi waliowachagua na siyo vinginevyo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari baada ya kuchukua fomu na kurejesha Makao Makuu ya CCM, Spika Ndugai alisema kuwa amefanya hivyo kwa kuzingatia utaratibu wa chama chake.

"Ni utaratibu wa chama chetu wa kidemokrasia nafasi hii inajazwa na wanaopendekezwa na vyama vyao vya siasa na kama chama changu kitanipa ridhaa ya kugombea nafasi hii, nikiwa Spika nitahakikisha tutaongea na wananchi kuhusu vipaumbele vyetu, fikra zetu na mambo mengine yanayofanana na hayo," alieleza Ndugai.

Kwa upande wake, Naibu Spika ambaye anatetea nafasi hiyo, alisema kuwa anaomba nafasi hiyo ili awatumikie Watanzania katika miaka mitano mingine ya Bunge la 12.

"Natumaini Bunge hili wabunge watatumia nafasi yao vizuri ya kuwawakilisha wananchi kwa kuikumbusha serikali ahadi zake katika ilani yake pamoja na kero mbalimbali zilizopo katika majimbo yao, ili zifanyiwe kazi," alisema.

Akizungumzia Bunge la 11, alisema moja ya tatizo kwa wabunge katika bunge hilo, ni kutofahamu kanuni na taratibu za uendeshaji wa mhimili huo.

"Katika Bunge la 11, mwanzoni lilikuwa gumu nilikiwa nakumbana na tatizo la wabunge wengi kutofahamu kanuni za bunge hali ambayo ilikuwa inasababisha wengine kuingilia wenzao wakati wakiwa wanazungumza," alisema Dk. Tulia.

Alisema anatoa rai kwa wabunge wa Bunge la 12, kuzisoma na kuzishika kanuni na taratibu mbalimbali ili kuondokana na tatizo hilo.

Alipoulizwa sababu za kutogombea nafasi ya uspika, Dk. Tulia alisema kuwa hivi sasa amepata jukumu jingine la kuwa Mbunge wa Mbeya Mjini, hivyo ana wajibu pia wa kuwatumikia wapiga kura wake.

"Sio kama naogopa kugombea nafasi ya uspika, mimi siyo muoga kabisa ndio maana hata leo hii mimi ni mbunge wa jimbo ambalo lilikuwa na tatizo kubwa na halijawahi kuongozwa na mwanamke, lakini nimeona kwa wakati huu nafasi hii ndiyo itakayonifaa," alifafanua.

Katibu Msaidizi Mkuu wa Organaizesheni ya CCM Taifa, Solomon Itunda, alisema uchukuaji na urejeshaji fomu ulianza juzi na ulihitimishwa jana saa 10:00 jioni.

"Watu ambao nilikuwa na taarifa nao kwa leo (jana) ni hawa wawili ambao tayari wamechukua wamejaza na kurejesha fomu, fomu moja ilikuwa inatolewa kwa Sh. 500, 000," alisema Itunda.

Katika hatua nyingine, Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM, itafanya kikao chake Novemba 6 mwaka huu jijini Dodoma kwa ajili ya kupitisha majina ya walioomba nafasi ya Spika wa Bunge na naibu wake huku kikiongeza muda wa uchukuaji fomu hadi leo saa 10 jioni.

Katibu Mkuu wa chama hicho, Dk. Bashiru Ali, alisema jana kuwa mbali na kupitisha majina hayo, kikao hicho pia kitapokea taarifa ya awali ya utekelezaji wa mpango wa CCM wa uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

"Agenda ya pili ni kupitia majina ya wanachama waliomba nafasi ya uspika katika Baraza la Wawakilishi na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na muda umeongezwa kwa uspika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Uwakilishi zoezi limekamilika na vikao vya awali vimefanyika," alisema.

■ **Imeandikwa na Paul Mabeja na Augusta Njoji**







Open Job Vacancies /Nafasi za kazi

**HBS** is a **NECTA** registered private Pre-school and Primary school located in Kigamboni, Dar es Salaam. The school is expanding and currently hiring the following posts:

- Teaching Volunteers (4)*
- Deputy Heads of School (2)
- Deputy Heads, Pre and Primary (2)
- Pre-school/Nursery and Primary School Teachers (10)
- Receptionists / Admin officers (2)
- Head of Premises & Transportation (1)
- Electrical / Mechanical Engineer (2)
- Accountant (1)
- School bus Drivers (10)
- Pre-school Helpers (6)
- Chefs/Cooks (3)

For job descriptions and qualifications please visit our website www.hbs.ac.tz or our social media sites Instagram: hbs.tanzania facebook: Hannah bennie-schools. Please send your applications to hr@hbs.ac.tz copy hr.hbs.tz@gmail.com.

**Deadline 15th November 2020.**

**Due to volumes of calls, we are unable to respond to calls related to this Job advert, please raise all your enquiries via email addresses above.**

# Mgombea wa ubunge aachiwa kwa dhamana

**Na Restuta Damian,**
BUKOBA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera imewaachia kwa dhamana ya Sh. milioni tano kila mmoja washtakiwa sita akiwamo aliyekuwa mgombea wa ubunge wa Bukoba Mjini (CHADEMA), Chief Kalumuna, kwa mashtaka ya uharibifu wa mali za serikali.

Akitoa tamko baada ya mawakili pande mbili kuridhia kuwa hakuna pingamizi la dhamana kati yao, Hakimu Mkazi Joseph Luambano alisema kila mshtakiwa anatakiwa kuwa na wadhamini wawili wenye kuaminika.

Awali, Wakili wa Serikali Haruna Shomari, akishirikiana na Susan Richard na Juma Wahona, aliwataja washtakiwa, mbali na Kalumuna (39) kuwa ni Ismail Kamala (49) Jovitus Rubangaiza (27), Antidius Mtajaiwa (46), Victor Shelejei (54), Softened Mrashobelwa (41) na Abdmarick Audax(36).

Shomari alidai kuwa Oktoba 21, mwaka huu, siku ya kuapisha mawakala wa vyama vya siasa, washtakiwa wa walifanya vurugu katika eneo la uwanja wa Kaitaba na kuharibu vioo vya jengo la ofisi ya Halmashauri ya Manispaa Bukoba.

Pia alidai kuwa washtakiwa hao hawakutii amri halali ya kuondoka eneo walilokuwa wamekusanyika na kuharibu kioo cha magari aina ya Toyota Landcruiser yenye namba za usajili PT 1835 na PT 3635.

Mbali na vioo, alidai kuwa washtakiwa walivunja boneti ya mbele ya gari la Halmashauri ya Manispaa Bukoba pamoja na kuvunja kioo cha gari la abiria na kushambulia na kudhuru mwili na kujeruhi uso wa Mrakibu Mwandamizi wa Polisi (SSP) Babu Sanale.

Aidha, Wakili Shomari alidai upelelezi umekamilika hakuna pingamizi upande wa Jamhuri.

Upande wa utetezi uliyokuwa na mawakili Dunstan Rutagaiwa na Felix Mtasingwa, walidai kuwa wateja wao wako tayari kutekeleza masharti ya mahakama ambayo yameambatana na wadhamini wawili wenye kuaminika.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi (katikati), akipata maelezo kutoka kwa Mdhibiti wa Bandari wa Shirika la Bandari Zanzibar, Majaliwa Abdalla Rashid, wakati alipotembelea Bandari ya Malindi, jana. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Vumbi latimka kinyang'anyiro umeya, naibu meya, wenyeviti halmashauri

**Na Waandishi Wetu**

KINYANG'ANYIRO cha nafasi ya mwenyekiti, makamu mwenyekiti na umeya wa Halmashauri kimeanza kutimua vumbi katika maeneo mbalimbali huku madiwani wateule wakijitosa kuchukua fomu.

Mchakato huo unafanyika kutokana na kumalizika kwa uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani uliofanyika Oktoba 25, mwaka huu.

Katika majimbo ya Kahama Mjini. Msalala na Ushetu, madiwani wateule 19 wamejitokeza kugombea nafasi ya Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri kutoka majimbo hayo.

Akitoa taarifa za uchukuaji wa fomu za kugombea nafasi hizo jana, Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kahama, Emmanuel Mbamange, alisema waliochukua fomu wajipime kuendana na kasi ya maendeleo yanayotarajiwa na wananchi.

Alisema waliojitokeza kuchukua fomu hizo, watatu ni kutoka Msalala, saba Ushetu na tisa Mji Kahama.

Mbamange aliwataja waliojitokeza Kahama Mji kuwa ni Abel Shija, Benard Mahongo, Yahya Bundala, Joseph Albert, Scolastika Bebeto na Hamidu Kapama.

Waliochukua kwa Halmashauri ya Msalala ni Mibako Mabubu, Berenadict Manwali na Flora Sagasaga na Ushetu Tabu Katoto, Emmanuel Makashi, Msafiri Mnyili na Mkomba Daudi.

**SONGEA MOTO**

Katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma, madiwani wateule wanane wamejitokeza kuchukua fomu za kuwania kuteuliwa na vikao vya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kugombea nafasi ya umeya.

Kaimu Katibu wa CCM Wilaya ya Songea Mjini, Rehema Hussen, alisema kuwa chama hicho kimefungua milango kwa madiwani wateule kuchukua fomu za kuwania nafasi ya umeya na unaibu meya.

Hussen ambaye ni Katibu wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Wilaya ya Songea Mjini, aliwataja madiwani hao wateule na kata zao kwenye mabano kuwa ni Mathew Ngalimanayo (Mjini), Michael Mbano (Msamala), Issa Mkwawa (Matogoro) na Yobo Mapunda (Lilambo).

Aliwataja wengine kuwa ni Festo Mlelwa (Seed Farm), Mussa Mwakaje (Mateka), Hajira Kalinga (Mfaranyaki) na John Ngonyani wa Kata ya Subira wakati aliyechukua fomu hadi jana kuwania unaibu meya ni Judith Mbogoro, Diwani Mteule wa Kata ya Matarawe.

Katibu huyo alisema kuwa katika Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Manispaa lililopita nafasi ya umeya ilikuwa inashikiriwa na Alhaji Abdul Mshaweji ambaye alikuwa Diwani wa Kata ya Subira. Mshaweji aliangushwa kwenye kura za maoni.

Naye Katibu wa CCM Wilaya ya Songea Vijijini, Mohamed Lawa, alisema katika Halmashauri ya Songea, aliyekuwa Makamu Mwenyekiti, Menas Komba ambaye ni Diwani Mteule wa Kata ya Matimira amechukua fomu ya kuomba kuwania nafasi ya mwenyekiti.

Lawa aliongeza kuwa kwa nafasi ya makamu mwenyekiti, aliyechukua fomu ni Simon Kapinga ambaye ni Diwani Mteule wa Kata ya Lilai Muhukuru.

Katika Halmashauri ya Wilaya ya Madaba, alimtaja aliyechukua fomu ya kuomba kuwania nafasi ya mwenyekiti ni Vistus Mfikwa, ambaye ni Diwani Mteule wa Kata ya Mkongotema.

Mfikwa anatetea nafasi hiyo aliyokuwa akiishikilia katika Baraza lililopita na mwingine aliyechukua kuwania nafasi hiyo ni Teofanes Mlelwa ambaye ni Diwani Mteule wa Kata ya Wino.

■ **Imeandikwa na Shaaban Njia (KAHAMA) na Gideon Mwakanosya (SONGEA).**

# TRA yakamata shehena ya sukari

**Na Ambrose Wantaigwa,**
TARIME

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imekamata shehena ya bidhaa mbalimbali, ikiwamo sukari katika mpaka wa Sirari wilayani Tarime mkoani Mara.

Mamlaka hiyo imesema sukari iliyokamatwa ni tani14 iliyokuwa ikiingizwa nchini kwa kutumia njia zisizo rasmi.

Ofisa forodha katika kituo cha mpakani Sirari, Allan Maduhu, alisema hayo wakati akitoa taarifa ya ukaguzi kwa Mkuu wa mkoa wa Mara, Adam Malima, aliyefanya ziara ya kushtukiza katika mpaka huo.

Alisema miongoni mwa bidhaa zilizokamatwa katika oparesheni iliyofanyika mwishoni mwa Oktoba ni lita 9,000 za mafuta ya kula na mamia ya mifuko ya saruji zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 200. Alisema kwa kutumia kikosi kazi cha kuzuia magendo katika eneo hilo, wamebaini mitandao ya wafanyabiashara wasio waaminifu ambao sasa wanatumia waendesha pikipiki kuvusha shehena kubwa ya magendo.

"Hivi sasa baadhi ya wafanyabiashara wanatumia vijana wanaoendesha pikipiki kwa mwendo kasi kupitia njia za panya ili kukwepa vizuizi halali vya maofisa wa TRA mpakani hapa," alisema Maduhu.

Kwa upande wake, Malima alisema amesaini kibali kuwezesha bidhaa hizo zilizokamatwa na ambazo zinaweza kuharibika kwa muda mfupi kugawiwa katika taasisi za serikali. Katika hatua nyingine, aliagiza idara hiyo kuhakikisha inakomesha tabia ya kukwamisha malori yote yanayobeba milipuko katika mpaka huo kwa kuwa yanaweza kusababisha milipuko.

"Lazima hatua za haraka zichukuliwe kuhakikisha malori yote yanayobeba milipuko yakaguliwe kwanza kama yamefungwa vifaa vya kuzima moto, na yasisubirishwe kwa muda mrefu eneo la mpakani," alisema Malima.

Aliwataka wafanyabiashara wilayani Tarime kuwa wazalendo kwa kulipa kodi mbalimbali za serikali, na kuepuka kuingiza bidhaa kwa njia haramu kwa kuwa wanachangia kuua uchumi na viwanda vya Taifa.

## Waziri aipa mwezi SUMA JKT ujenzi Hospitali ya Uhuru

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, ameliagiza Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT) kukamilisha ujenzi wa Hospitali ya Uhuru ifikapo Desemba 5, mwaka huu.

Sambamba na hilo, amemwagiza Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Kessy Maduka, kuanza kuandaa wataalamu watakaofanya kazi kwenye hospitali hiyo ili kuanza kutoa huduma baada ya kukamilika ujenzi wake.

Akikagua maendeleo ya ujenzi wa hospitali hiyo iliyopo wilayani Chamwino jana, Waziri Jafo alisema licha ya ujenzi huo kuendelea vizuri, lakini unapaswa kukamilika kwa wakati ili dhamira ya Rais John Magufuli ifikiwe.

"Leo (jana) nimekuja kukagua hapa na binafsi naona kazi inaendelea vizuri,ila tatizo ninaloona hapa ilikuwa kuchelewa kwa upatikanaji wa material, lakini nafurahi kuwa tatizo hilo limetatuliwa na kiasi cha Sh. bilioni 1.2 kimeletwa ili kumalizia kazi hii,hivyo hakuna sababu ya kutokamilika,kazi iendelee na Desemba 5 ikamilike" alisema.

Alimuagiza Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, kufika hospitalini hapo Jumatatu ili kuona kama vifaa vimeshafika na ujenzi unaendelea.

"Mara ya mwisho nilipokuja hapa nilisisitiza wataalam kutumia vifaa vinavyozalishwa hapa nchini ili kulinda viwanda vyetu na kuwezesha upatikanaji wa ajira kwa wananchi wetu,hili mhakikishe mnalitekeleza," alisisitiza Jafo.

Akitoa taarifa ya ujenzi huo,Msanifu ujenzi wa SUMA JKT, Girimu Kanansi, alisema mradi huo unatekelezwa kwa gharama ya Sh.Bilioni 3.99 ambapo ujenzi kwa sasa umefikia asilimia 90.

Hata hivyo, alisema wanakabiliwa na tatizo la kusuasua kwa upelekaji wa vifaa vya ujenzi, ukosefu wa mchanga na kokoto kwa wakati.

"Tukuahidi tutakamilisha ujenzi huu kwa muda uliotuambia,changamoto hizo zilikuwepo mwanzoni lakini kwa sasa tumeambiwa kila kitu kipo sawa," alisema.

Katika hatua nyingine, Waziri Jafo aamekagua ujenzi wa barabara za Mji wa Serikali Mtumba na kumwagiza Mkandarasi wa Kampuni ya China Hainan International Cooparation (CHICO) kutotumia kigezo cha ugonjwa wa Corona kama sababu ya kutokamilisha kazi hiyo kwa wakati.

"Mkataba hapa unataka kazi hii ikamilike Julai 2021,naomba iwe hivyo hakuna justification ya Covid hapa,angalieni msimu wa mvua unavyoenda,hapa Disemba ni kipindi cha mvua sasa mkilegalega hapa huko mbele itakuwaje?" alihoji.

Alisema hajaridhishwa na kasi ya ujenzi inavyoenda hivyo kumtaka mkandarasi kupeleka vifaa vyote vinavyohitajika ili kazi iende haraka na kukamilika kwa wakati.

"Hapa sio kwa sababu mkandarasi huyu ana jina kubwa ndio afanye anavyotaka hapana, msilete ubishororo wakati nikiangalia kazi haiishi, malizeni kazi tena kwa kiwango kinachotakiwa kitaalam, sio barabara inajengwa leo muda mfupi lami inavimba hapana," alisisitiza.

Awali, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), Mhandisi Victor Seff, alisema barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 40 inajengwa kwa kiwango cha lami kwa gharama ya Sh. bilioni 88.1 na imefanikiwa kutoa ajira 240.

"Mradi huu ulianza rasmi Februari mwaka huu na unategemewa kukamilika Julai 202. Katika utekelezaji wa mradi huu changamoto mbalimbali zilijitokeza ikiwamo uwapo wa Covid-19, mvua kubwa za masika na upatikanaji wa changarawe katika machimbo ya Mahomanyika," alisema.

# Wanusurika kifo gari kugonga nyumba

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

WATU watatu, wakiwamo mume na mke ambao ni wamiliki wa duka la dawa za binadamu mjini hapa, wamenusurika kifo baada ya gari kuacha njia na kuingia dukani na kusababisha uharibifu ikiwamo nyumba kubomoka.

Gari hilo lenye namba za usajili T 529 AGH linalomilikiwa na Onesmo Nzella, lililokuwa limebeba mpunga kutoka Lugunga Wilaya ya Mbongwe kuja mjini hapa, liliacha barabara na kugonga dereva bajaji ambaye jina lake halikujulikana na kuingia katika duka hilo linalomilikiwa na Elizabeth Anthon (38).

Ajali hiyo ilitokea juzi majira ya saa nne za usiku baada ya dereva wa gari hilo jina halikupatikana kushindwa kukata kona ya kuingia kwenye barabara ya kwenda Hhongolo kwenye mashine za mpunga.

Kutokana na kuhindwa kukata kona, gari hilo liligonga bajaji na kuvamia nyumba, kujeruhi na kusababisha uharibifu wa mali pamoja na nyumba kubomoka.

Mmiliki wa duka hilo alisema wakati akiwa ndani ya nyumba, aliona gari likiingia ndani na ukuta wa nyumba ukaanguka na watu waliokuwapo eneo la tukio kujazana.

Alisema baada matofali kuanza kudondoa, aliona gari hilo likiingia ndani ya nyumba yao ya biashara lakini hakuna mtu yeyote aliyafariki dunia bali baadhi ya watu walipata majeraha madogo madogo na kupelekwa Hospitali ya Wilaya ya Kahama.

Hata hivyo, Anthon alisema chanzo cha ajali hiyo ni dereva kuendesha kwa mwendo kasi, hivyo gari hilo kumshinda wakati wa kukata kona hali iliyosababisha kuacha njia ya kuingia katika nyumba ya mtu.

Mmoja wa mashuhuda ambaye pia ni mume wa Anthon, Dickson Musa (41) alisema ajali nyingi zimekuwa zikitokea mara kwa mara katika eneo hilo na kusababisha maafa na watu wengi kujeruhiwa.



Gari aina ya Fuso lenye namba za usajili T 529 AGH, linalomilikiwa na Onesmo Peter Nzela likiwa limegonga nyumba na kuingia ndani na kujeruhi watu watatu katika kata ya Majengo, Halmashauri ya Mji wa Kahama jana. **PICHA: NEEMA SAWAKA**

# Makada CHADEMA kortini madai ya uhujumu uchumi

**Na Edna Alex,** SINGIDA

WATU wapatao 20 wanaosadikiwa kuwa ni wafuasi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi mkoani hapa na kusomewa mashtaka ya kesi ya uhujumu uchumi.

Wakisoma mashtaka dhidi ya washtakiwa, jopo la mawakili wa serikali kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, wakiongozwa na Wakili Caren Mrango mbele ya Hakimu Mkazi Consolata Singano, walidai kuwa washtakiwa kwa nyakati tofauti kati ya Oktoba 29 na Novemba 1, 2020 wakiwa na nia ovu, walitenda makosa matatu yanayohusiana na uhujumu Uchumi.

Mrango aliyataja makosa hayo ni kuratibu na kuongoza genge lenye nia ovu ya kuhamasisha vurugu kupitia maandamano, kula njama kwa lengo la kutenda kosa na kufanya mkusanyiko bila kuwa na kibali.Aliwataja washtakiwa ni Jingu Jackson, Emanuel Lissu, Wilson Kidaghoo, Gideon Murya, Steven Mangu, Mika Muna, Joseph Daffi, Swalehe Mangu, Morinyo Muhanja na Benedict John.

Wengine ni Salum Kiduka, Ibrahim Madaraka, Juma Hisu, Lightnes Masoud, Mashavu Ibrahim, Esther Kiwali, Debora Shaban, Bahati Sambaa, Christina Hamis na Noela Lemoyani.

Washtakiwa walisomewa mashtaka hayo na kutakiwa kutojibu chochote kutokana na Mahakama hiyo kutokuwa na mamlaka ya kuendesha shauri hilo. Kesi hiyo ambayo haina dhamana, iliahirishwa na washtakiwa kurudishwa mahabusu hadi itakaposomwa tena Novemba 13, mwaka huu.


UNHCR
United Nations High Commissioner for Refugees
Haut Commissariat des Nations Unies pour les réfugiés

TENDER NOTICE

1. INVITATION TO BID No: ITB/2020/SUP/031: FOR THE ESTABLISHMENT OF FRAME AGREEMENT FOR THE SUPPLY OF MULTIPURPOSE SOAP

1.1 Background:
The Office of the United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR), Representation Office in Dar es Salaam invites you to submit firm offers for Establishment of multiple Frame Agreements for the supply of Multipurpose Soap.

1.2 Eligibility:
**Manufacturers/Factories based in Tanzania** duly registered with relevant government authorities, with sound financial basis, relevant experience, reputed clientele and with knowledge of how to meet UNHCR's requirements are invited to participate in the bidding process.

1.3 Crucial dates for this Request for Proposal

| | |
|---|---|
| Pre-bid Conference at UNHCR Offices in Masaki | Monday 16th November 2020 10.00 Hours EAT |
| Deadline for Receiving Requests for Clarification | Monday 16th November 2020 18.00 Hours EAT |
| Deadline for Submission of Offers | Monday 30th November 2020 16.00 hours EAT |

INVITATION TO BID No: ITB/2020/SUP/038: FOR THE ESTABLISHMENT OF FRAME AGREEMENT FOR THE SUPPLY OF UNDERWEAR

2.1 Background:
The Office of the United Nations High Commissioner for Refugees (UNHCR), Representation Office in Dar es Salaam invites you to submit firm offers for Establishment of multiple Frame Agreements for the supply of Underwear.

2.2 Eligibility:
**Manufacturers, authorized resellers, wholesalers,** or traders based in Tanzania duly registered with relevant government authorities, with sound financial basis, relevant experience, reputed clientele and with knowledge of how to meet UNHCR's requirements are invited to participate in the bidding process.

2.3 Crucial dates for this Request for Proposal

| | |
|---|---|
| Deadline for Receiving Requests for Clarification | Monday 16th November 2020 18.00 Hours EAT |
| Deadline for Submission of Offers | Monday 30th November 2020 16.00 hours EAT |

The tender documents can be accessed through the following link:

https://drive.google.com/drive/folders/1hhIVmcvPeaJPoII25cT9IL-mZseIc63p?usp=sharing

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Halmashauri ziongozwe na wenyeviti, mameya wenye uwezo kitaaluma

**CHAMA** Cha Mapinduzi (CCM) kimeanza mchakato wa kuwatafuta spika, naibu spika, wenyeviti wa halmashauri za miji na wilaya na mameya wa majiji na halmashauri za manispaa.

Hatua hiyo inatokana na matokeo ya uchaguzi mkuu wa Jumatano, ambao umekipatia ushindi mkubwa, hivyo kukiwezesha sasa kuongoza halmashauri zote kutokana na kuwa na idadi kubwa ya madiwani.

Ingawa sheria inaruhusu mtu yeyote kupitia chama chochote cha siasa chenye usajili wa kudumu kugombea nafasi ya spika, lakini kwa nafasi zote za wenyeviti na mameya zinabakia kugombewa na madiwani wa CCM.

Tunatarajia kwamba madiwani wengi wa CCM watazichangamkia nafasi hizo, lengo likiwa ni kusimamia halmashauri hizo ziwapatie wananchi maendeleo.

Ikumbukwe kwamba kwenye halmashauri ndiko wanapoishi wananchi wengi na ndipo wanapotegemea kupelekewa maendeleo, hivyo, kuna haja ya kuwapata viongozi (mameya na wenyeviti) ambao wana uwezo wa kusimamia upatikanaji wa huduma muhimu hususan za kijamii kwa wananchi.

Wakati huu wa mchakato wa kuwapata viongozi hao, wengi watajitokeza kwa ajili ya kuchaguliwa, huku baadhi wakitanguliza mbele maslahi binafsi badala ya maslahi ya umma.

Ili wananchi wapelekewe maendelo kwa kasi inayostahili, ni wajibu wa madiwani ambao ndio wanaowachagua viongozi hao kuhakikisha kwamba wanatanguliza mbele maslahi ya umma kwa kuwachagua wagombea wachapakazi na wenye elimu ya kutosha ya kuibua na kusimamia miradi yenye tija.

Elimu ya kutosha hainabudi kuwa kigezo kikubwa kwa sababu watendaji na wataalamu wa halmashauri zetu ni watu wasomi kuanzia kwa wakurugenzi hadi wakuu wa idara, hivyo wanahitaji kusimamiwa na mameya wa wenyeviti ambao ni wasomi.

Kimsingi, viongozi hao wakiwa wasomi, wataweza kuzielewa ripoti zinazoandaliwa na watendaji, na pale watakapoona kasoro watazikosoa na hata kuzikataa.

Vilevile, kuwa na mameya na wenyeviti wasomi, itakuwa rahisi kusimamia fedha zinazopelekwa katika halmashauri kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Kuna fedha kadhaa zinazopelekwa katika halmashauri, zikiwamo za kutoka serikali kuu zikiwamo za Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), mashirika ya kimataifa kama la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Maendeleo (UNPD) pamoja na wadau wengine wa halmashauri hizo.

Katika hali hii, suala la kuwa na mameya na wenyeviti wenye elimu ya kutosha haliepukiki katika usimamizi wa fedha hizo, ili miradi itekelezwe kulingana na thamani halisi ya fedha.

Kama madiwani watapuuza ushauri huu na kuwachagua watu wenye maslahi binafsi, basi wafahamu kuwa baada ya miaka mitano wapigakura wao hawataona mabadiliko yoyote ya kimaendeleo, badala yake wataishia kulalamika kuwa fedha zilizopelekwa kutekeleza miradi zilichakachuliwa.

Huko nyuma tulishuhudia katika halmashauri nyingi wenyeviti/mameya na madiwani wao wakiwa mstari wa mbele katika kudai posho na kuingilia utendaji wa wataalamu katika mambo yasiyo na tija, huku halmashauri zao zikishindwa kusimamia miradi na matumizi ya fedha.

Matokeo yake ni kuwa baadhi ya halmashauri zilijikuta zikipata hati chafu kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Ni matumaini yetu kwamba utendaji wa halmashauri utakuwa na tija na ufanisi ikiwa madiwani watazingatia ushauri wetu wa kuwachagua wenyeviti na mameya wasomi, waadilifu na wachapa kazi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Uamuzi kususia uchaguzi mkuu waweza kuwa sawa, lakini...

Na Sabato Kasika

**SIKU** chache baada ya uchaguzi mkuu kumalizika, Chama cha Wananchi (CUF), kimetangaza maamuzi magumu yanayoeleza nia ya kutoshiriki tena uchaguzi mkuu hadi itakapopatikana Tume Huru ya Uchaguzi.

CUF inatangaza kuwa inaelekeza nguvu zake katika kupigania katiba mpya yenye misingi ya demokrasia na utawala bora, huku pia ikijipanga kuanzisha mazungumzo na jumuiya za kimataifa.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa CUF, Profesa Ibrahim Lipumba, mazungumzo hayo yatalenga zaidi katika kuiomba kuisaidia Tanzania kujenga misingi ya kudumu ya demokrasia na utawala bora.

Hayo ni sehemu yaliyokuwamo katika tamko la chama hicho lililotolewa jijini Dar es Salaam juzi na mwenyekiti huyo kwamba kuanzia sasa kwa kushirikiana na wadau wengine watajumuika kufanikisha lengo hilo.

CUF inachukua uamuzi huo, huku kukiwapo na madai ya muda mrefu ya baadhi ya vyama vya upinzani nchini ya kutaka kuundwa kwa tume huru ya uchaguzi, ambayo inaamini inaweza kutenda haki katika uchaguzi.

Vilevile ni karibu miaka 30 sasa tangu kuwapo hatua mbalimbali za kudai Tume Huru ya Uchaguzi, ambazo mara kadhaa zimekuwa zikiibuka na kupotea kwa nyakati tofauti bila mafanikio.

Kwa wale wanaokumbuka safari ya kutaka tume hiyo, ilianza mwaka 1991 baada ya Rais wa Awamu ya Pili, Ali Hassan Mwinyi kuunda tume iliyoongozwa na Jaji Francis Nyalali (marehemu), kukusanya maoni kuhusu mfumo wa vyama vya siasa, lakini kuliwapo na mapendekezo ya kubadilishwa kwa tume ya uchaguzi ili iwepo yenye kukidhi mfumo wa demokrasia ya vyama vingi.

Ni tangu mwaka 1991, harakati za kutaka tume hiyo zilianza, lakini hadi sasa imeendelea kuwa ile ile, Prof. Lipumba alitakiwa kulitambua hilo mapema na kuchukua hatua hiyo badala ya sasa hata kabla ya uchaguzi wa mwaka 1995.

Mwaka 1995 ndipo ulipofanyika uchaguzi wa kwanza ndani ya mfumo wa vyama vingi na hadi sasa umefika wa sita kwa kusimamia wa tume ambayo Jaji Nyalali alishauri ibadilishwe kulingana na mazingira ya sasa ya kisiasa.

Kwa uamuzi wa Prof. Lipumba na chama chake, ninaweza kusema ni sawa, lakini hatua kama hiyo alipaswa kuichukua muda mrefu na hasa kwa kuungana na vyama vingine kudai tume huru kuliko kuwa pekee yake.

Haimaanishi kwamba amechelewa, bali ni muhimu kuungana na vyama vingine vyenye lengo moja, ili kuhakikisha inakuwapo tume huru na kuondoa malalamiko yote ambayo hujitokeza kabla na baada ya uchaguzi.

Lengo ni lazima liwe moja kwa sababu vipo baadhi ya vyama visivyo na wawakilishi bungeni ambavyo vimewahi kukaririwa na vyombo vya habari vikipinga madai ya vyama vingine vya upinzani ya kutaka tume huru.

Kwa upande wa suala la katiba mpya yenye misingi ya demokrasia na utawala bora, CUF ilikuwa miongoni mwa vyama vilivyounda Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) wakati ule wa Bunge Maalum la Katiba, mwaka 2014.

Wakati vikao vya bunge hilo vikiendelea, vyama hivyo ambavyo ni pamoja na CHADEMA, NLD, na NCCR-Mageuzi, vilisusia bunge hilo na kuamua kwenda mitaani kudai katiba hiyo.

Hata hivyo, baadaye Prof. Lipumba alijiweka pembeni wakati vyama vingine vikiendelea na harakati hizo ingawa hadi sasa hazijazaa matunda ya kupatikana tume huru na katiba mpya.

Lakini jambo la msingi ni kwamba, bado kuna haja ya vyama kuungana kwa ajili ya kuendelea madai hayo kuliko kila chama kufanya kivyake, kwa kuwa hali hiyo itakuwa kana kwamba hakuna uzito wowote.

Waswahili wana msemo kwamba, 'umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu', hivyo kuendelea kutengana katika maamuzi hayo kunaweza kuchelewesha mikakati ya vyama kudai tume huru na katiba mpya.

Madai ya kutaka tume huru ya uchaguzi na katiba mpya vinawezaa kupata msukumo kwa nguvu za pamoja za vyama vya upinzani, kuliko kila kimoja kudai kivyake kana kwamba vingine havihusiki.

## CIP kutafiti sababu za wapigakura wachache

**Na Christina Mwakangale**

KITUO cha Sera cha Kimataifa barani Afrika (CIP), kimesema kwamba kinafanya utafiti kubaini sababu za kuwapo kwa idadi ndogo ya wapigakura, hususani vijana, kwenye uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), ilisema katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu, kati ya wapigakura 29,188,347 waliojiandikisha wapigakura 14,830,195 hawakujitokeza kupiga kura, huku 15,891,950 wakipiga kura.

Mkurugenzi Mtendaji wa CIP, Omar Mjenga, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, akizungumza na waandishi wa habari na kutoa taarifa ya awali kuhusu uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Mjenga alisema watazamaji wa kituo hicho walibaini kuna elimu duni kuhusu uchaguzi na umuhimu wa upigaji kura, baadhi ya wasimamizi kutofahamu majukumu yao na uwapo wa idadi kubwa ya vyombo vya ulinzi na usalama, inayoweza kuwa kati ya sababu ya ushiriki mdogo wa wapigakura. "Uelewa kuhusu siku ya upigaji kura ambayo ilitangazwa ni siku ya mapumziko, Oktoba 28, ulikuwa mkubwa. CIP kwa kushirikiana na NEC, ZEC tutafanya utafiti kuhusu uchaguzi huu. Licha ya kuwapo kwa idadi kubwa ya waliojindikisha kwa ajili ya kupiga kura, kwa nini hawakupiga kura." alisema Mjenga na kuongeza:

"Katika vituo walijitokeza watu wachache, CIP tunahitaji kufanya utafiti kwa nini watu milioni 14 karibu asilimia 50, hawakujitokeza kupiga kura. Kwa nini mtu ajiandikishe na amesikiliza maelekezo, sera, siku ya kupiga kura asipige kura na kulikuwa na amani na utulivu."

Mjenga alisema taarifa kutoka wa watazamaji wa kituo hicho, ni kwamba kulikuwa na malalamiko ya watu kuwa uwapo wa idadi kubwa ya vyombo vya ulinzi na usalama, kulisababisha woga kwa baadhi na kutoshiriki uchaguzi.

"Kuwapo kwa askari kwenye kituo maana yake ni kwa ajili ya usalama wa wapigakura na si vinginevyo, watu walisema vyombo vya usalama vilikuwa sababu ya idadi ndogo ya wapigakura," alisema. Aidha, Mjenga alisema watazamaji walibaini baadhi ya wasimamizi wa uchaguzi hawakujua kanuni na hatua za kufuatwa katika usimamizi wa uchaguzi, na kwamba kunahitajika wasimamizi walio na ujuzi na kupewa mafunzo kwa ufasaha kwa uchaguzi ujao.

Alisema kituo pia kilibaini mambo kadhaa kwenye mikoa 17 nchini ambako kilikuwa na watazamaji, ikiwamo mazingira ya wakati wa kupiga kura, kuhesabu kura na kutangaza matokeo.

"Taarifa hii ipo katika maeneo matano, kabla ya uchaguzi na baada ya uchaguzi. kampeni zilikuwa za amani na zenye mpangilio na kulikuwa na ushindani mkubwa kati ya Chama Cha Mapinduzi (CCM). Tulibaini kulikuwa na mawakala wa vyama vya siasa vitatu katika vituo vingi, hasa CCM, CHADEMA, ACT-Wazalendo, na badhi ya vituo mawakala walichelewa kufika," alisema Mjenga.

Mjenga alisema kwamba kulikuwa na idadi kubwa ya wapigakura wanawake kwenye vituo vingi, licha ya baadhi ya vituo wanawake kudai kwamba waume zao waliwakataza kushiriki upigaji kura.

"Mkoani Kigoma, baadhi ya vituo kinamama waliogopa kujitokeza au walipomaliza kupiga kura walifuta wino katika kidole sana, ili asije akagombana na mume wake, akirudi nyumbani," alisema.

Pia alisema mkoani Lindi, kituo kimoja mmoja wa waangalizi alijeruhiwa kichwa, baada ya kutokea fujo na kufikishwa hospitalini na kushonwa nyuzi nane kichwani.

Mjenga alisema NEC pamoja na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) zijipange kutoa elimu kuhusu upigaji kura hasa kwa uchaguzi ujao ikiwamo kuwapa elimu ya kutosha wasimamizi wa uchaguzi kutambua majukumu yao.

Kituo hicho kilikuwa na watazamaji katika maeneo tofauti nchini, ikiwamo mkoa wa Mbeya, Arusha, Dodoma, Dar es Salaam, Iringa, Mwanza, Kilimanjaro na Kigoma. Mingine ni Mara, Mtwara, Lindi, Rukwa, Ruvuma, Tabora, Pemba na Zanzibar.



Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sera cha Kimataifa barani Afrika (CIP), Omar Mjenga, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu taarifa ya awali kuhusu uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28, mwaka huu. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

## Viongozi dini wataka matokeo yakubaliwe

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

VIONGOZI wa dini nchini wamewataka viongozi wa vyama vya siasa, kukubali matokeo ya urais yaliyopatikana katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, kwa kuwa wananchi ndio walioamua kupitia masanduku ya kupigia kura.

Vile vile, viongozi hao wameyataka mataifa ya nje kuacha kuingilia masuala ya nchini kwa kuwa matatizo ya Tanzania yatamalizwa na Watanzania wenyewe. Akizungumza jijini hapa jana, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maridhiano Taifa, Sheikh Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhadi Musa Salum, alisema baada ya uchaguzi kumalizika mshindi amepatikana, kinachotakiwa ni jamii kuendelea na maisha mengine.

"Niwaombe baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa vya upinzani, wanaopinga matokeo ya uchaguzi wakubali tu matokeo hayo kwani katika ushindani lazima mshindi mmoja apatikane, aliyechaguliwa na wengi ndio kastahili," alisema Sheikh Musa.

Alisema wao viongozi wa dini wanaendelea kumuomba Mungu amani ya nchi iendelee kuwapo kwa kuwa sifa ya Tanzania ni amani na utulivu.

"Nchi za wenzetu huko nje wanateseka na vita vya wenyewe kwa wenyewe, sisi hatutaki tufike huko, hivyo kama mtu haridhishwi na matokeo afuate taratibu za sheria za nchi," alisema.

Alisema kuwa jumuiya ya maridhiano pia inasikiliza malalamiko, na kuwaomba viongozi hao kuyapeleka yakatatuliwa kwa mazungumzo.

Hata hivyo, Sheikh Alhadi alisema Jumuiya hiyo inamshukuru Mungu nchi kuvuka salama katika uchaguzi mkuu na hatimaye kupatikana kwa rais mteule na viongozi wengine katika njia ya amani.

"Niwatake Watanzania kumshukuru Mungu kwa kuwa amejibu maombi yetu, tumekuwa tukimuomba atupe amani katika kipindi chote cha kampeni mpaka uchaguzi mkuu umeisha tumevuka salama," alisema.

Katibu Mkuu wa Jumuiya hiyo, Oswald Mlay, alisema licha ya kuwa uchaguzi umepita, wataendelea kuomba na kuhubiri amani.

"Viongozi wa dini kazi yetu ni kuendelea kuomba Mungu na kuhubiri amani, hivyo niwatake Watanzania waendelee kuliombea taifa," alisema Mlay.

Mlay, alisema mataifa ya nje yafanyie kazi ripoti ya waangalizi wa uchaguzi ambao walitoa taarifa kuwa uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28, mwaka huu ulikuwa huru na haki.

Mwisho

## CCM yatoboa siri ushindi Mwanza

**Na Richard Makore,** MWANZA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Mwanza kimetoa siri ya kujinyakulia ushindi kwenye uchaguzi mkuu katika majimbo yote tisa mkoani humo, kuwa ni ushirikishwaji wa wanachama kuanzia ngazi ya shina hadi mkoa ndiyo njia pekee iliyowasaidia.

Akizungumzia na Nipashe ofisini kwake jana jijini humo, Katibu wa CCM Mkoa wa Mwanza, Julius Peter, alisema njia pekee iliyowasaidia ni kuwashirikisha wanachama wote na kuwaunganisha viongozi wa ngazi zote. Alisema kila ngazi ya uongozi ilikuwa na kamati yake ya kutafuta ushindi na hatua hiyo ilikipatia ushindi chama kwa majimbo yote zikiwamo kata

Hata hivyo, alisema waliopoteza kata mbili na kunyakuliwa na CHADEMA ni sehemu ya demokrasia.

Pia, alisema majimbo ya Mwanza mjini ya Ilemela na Nyamagana yalikuwa yakinyakuliwa na upinzani mwaka 2010, lakini sasa yamerudi mikononi mwa CCM.

Akizungumzia matarajio baada ya ushindi, alisema kazi pekee iliyobaki ni kuwatumikia wananchi kwa ngazi zote za uwakilishi walizopata ushindi.

Alijigamba kwamba ni jambo jema kwa kiongozi kusimamia wanachama na kisha kuona ushindi unapatikana.

# Shirika lasaidia maziwa yatima unga kilo 600

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

WATANZANIA wametakiwa kuwa na moyo wa upendo na huruma kwa watoto yatima na ambao wanaishi katika mazingira magumu kwa kuwasaidia mahitaji muhimu ya kibinadamu.

Hatua hiyo itawawezesha kufarijika na kuishi kwa amani na furaha kama walivyo watoto wenye wazazi.

Wito huo ulitolewa juzi kwenye kituo cha kulelea watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu cha Chipole na Katibu wa Shirika lisilo la kiserikali la Saint Theresa Orphans Foundation (STOF), Moses Nyirenda .

Nyirenda alisema hayo alipokuwa akikabidhi maziwa ya unga maboksi 50 yenye maziwa makopo 600 yenye thamani ya Sh. milioni 12.

Alisema kusaidia yatima na watoto wanaoishi katika mazingira magumu ni miongoni mwa ishara njema ya kuwaonyesha upendo, wema, utu na huruma katika ustawi wao na jamii ijayo.

Nyirenda alisema watoto ambao wanaishi katika kituo hicho, wanatoka katika maeneo mbalimbali katika Mkoa wa Ruvuma ambapo familia zao hazina kipato, huku wengine wakiokotwa baada ya kutupwa na wazazi wao au kutelekezwa baada ya kuzaliwa.

Kutokana na hali hiyo, wanapaswa kusaidiwa mahitaji mbalimbali ili kuonyesha kuwajali na kuwathamini katika maisha yao.

Akielezea matumizi ya maziwa hayo, Mratibu wa STOF, Galus Mpepo, alisema yapo kwenye fomula ambapo kwa watoto wa kuanzia mwezi 0 hadi miezi 6, yako makopo 180, kuanzia miezi 6 hadi 12 ambayo ni fomula ya pili yapo makopo 300 na fomula ya tatu ambayo watoto kuanzia mwaka 1 na kuendelea yapo makopo 120

Garus alisema maziwa hayo yakitumika vizuri na kwa kuzingatia fomula yatawawezesha kuboresha afya za watoto hao na maziwa hayo yatatumika kwa zaidi ya miezi mitatu na kwamba muda wake wa kuharibika ni mwaka mmoja kutoka sasa.

Mlezi wa Kituo hicho, Sista Akwinata, akipokea msaada huo, alisema kituo hicho kilianzishwa mwaka 1963 na kwamba hadi sasa kimewalea watoto kutoka maeneo mbalimbali ya nchi ambao walitelekezwa baada ya kuzaliwa pamoja na wale wenye mazingira magumu

Sista Akwinata alisema hadi sasa kituo kina watoto 69 ambao wanaishi katika kituo hicho, hivyo wanashukuru kwa msaada walioupata kutoka STOF kwa kuwa utawawezesha kuboresha afya na maisha ya watoto hao.

# Abood ampongeza JPM ushindi wa kihistoria

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

MBUNGE Mteule wa Morogoro Mjini (CCM), Abdulaziz Abood, amempongeza Mwenyekiti wa chama hicho, Rais John Magufuli, kutokana na ushindi wa kimbunga alioupata kwenye Uchaguzi Mkuu uliofanyika wiki iliyopita.

Katika uchaguzi huo uliofanyika Oktoba 28, mwaka huu, Rais Magufuli aliibuka mshindi kwa kupata kura milioni 12.5 sawa na asilimia 84.4 akifuatiwa na mgombea wa Chadema Tundu Lisu aliyepata kura milioni 1.9 sawa na asilimia 13.

Akizungumza na gazeti hili jana, Abood alisema ushindi huo unadhihirisha Watanzania na wanachama wa CCM wanavyoridhishwa na kazi kubwa aliyoifanya Rais Magufuli katika kipindi cha miaka mitano ya urais wake.

Kwa mujibu wa Abood, hatua ya Rais Magufuli kuwashughulikia mafisadi, watumishi hewa, kutoa elimu bure, kujenga mradi mkubwa wa umeme wa bwawa la Nyerere Rufiji, kununua ndege, kujenga barabara nyingi za lami, kusimamia rasilimali madini zisitoroshwe nje ya nchi, kumempandisha chati kwa kiwango kikubwa.

"Hii ndiyo siri ya ushindi huu wa kihistoria kwa sababu Watanzania wengi wameona alivyojitoa kwa ajili ya kuwatumikia kwa moyo wake wote, hivyo wameona hawana zawadi nyingine ya kumpa zaidi ya kumpa ushindi wa kimbunga na kwa kweli alistahili ushindi mkubwa kama huu," alisema.

Alisema dalili za Rais Magufuli kupata ushindi wa kishindo kwenye uchaguzi mkuu uliopita zilianzia kuonekana tangu kwenye Mkutano Mkuu wa chama hicho baada ya wajumbe wote 1,822 wa mkutano huo kumpa kura ya ndiyo ili awe mgombea wa urais kupitia CCM.

Abood alisema binafsi ameguswa sana na utendaji kazi wa Rais John Magufuli akisaidiana na wasaidizi wake Makamu wa Rais na Waziri Mkuu kwani wamefanya makubwa kutekeleza Ilani ya Uchaguzi waliyoinadi kwenye uchaguzi wa mwaka 2015.

"Sisi wana CCM na Watanzania wote tunatembea kifua mbele na tuna kila sababu ya kufanya hivyo kwasababu



Wafanyakazi wa usafi wakizoa takataka zilizokuwa zimezagaa na kuhatarisha usalama wa afya za wafanyabiashara na wateja katika Soko la Buguruni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# TANAPA yataja chanzo moto Mlima Kilimanjaro

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa (TANAPA), limetaja chanzo cha moto uliozuka Mlima Kilimanjaro kuwa ni kichungi cha sigara na kuathiri sehemu ya mlima kilometa 95.

Aidha, TANAPA inatarajia ndani ya siku tatu kutoa taarifa ya tathmini ya hasara iliyosababishwa na moto huo na gharama halisi iliyotumika kwenye tukio hilo.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Kamishna wa Uhifadhi wa Shirika hilo, Dk. Allan Kijazi, alisema mpagazi na wenzake wawili walikuwa wakivuta sigara na kutupa kichungi hicho kwenye majani makavu na kusababisha moto huo.

Hata hivyo, alisema tayari hatua za kisheria zimechukuliwa na vyombo vya dola dhidi ya watuhumiwa wa kitendo hicho.

Dk. Kijazi ambaye pia ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, alisema moto huo kwasasa umedhibitiwa kwa asilimia 100 na jumla ya siku 17 zimetumika kukamilisha kazi hiyo.

Alisema moto huo ulizuka Oktoba 11, mwaka huu kwenye eneo la njia ya wageni itokayo Mandala kwenda Horombo katika eneo la Hona na nguvu kazi ya watu 1,899 imetumika kuzima moto huo.

"Moto ulianzia eneo ambalo kulikuwa na uoto ambao umekauka na kusambaa kwa kasi kubwa na jitihada za kuuzima kwa siku ya kwanza zilishindikana na ikaonekana kuna haja ya kuhusisha wadau wengine wengi na kuongeza nguvu ili kukabiliana na kasi ya kusambaa kwa moto," alisema.

Alisema kazi hiyo ilikuwa gumu na kulikuwa na uhitaji mkubwa wa maji, ndege na helikopta kutokana na maeneo mengi kutofikika kirahisi.

"Japo zoezi la kuzima lilifanikiwa ndani ya siku tano, baada ya hapo kulikuwa na kazi kubwa ya kuzima moto kwenye visiki, magogo na mboji, zoezi ambalo liliendelea kwa siku 12 na kuhitimishwa Oktoba 28, mwaka huu," alisema.

Dk. Kijazi alisema shughuli za utalii zinaendelea na sehemu iliyoathiriwa na moto haijaathiri shughuli za utalii kwenye mlima huo.

"Kwa tathmini tuliyoifanya inaonyesha sehemu ya mlima iliyoathirika ni kilometa 95, kama si nguvu za wadau wetu huenda hali ingekuwa mbaya zaidi, pamoja na moto kuzuka na jitihada tulizofanya, tulihakikisha muda wote shughuli za utalii haziathiriki," alisema.

Dk. Kijazi alisema kutokana na hali hiyo kwasasa wanajipanga kuandaa mpango maalum wa kukabiliana na majanga ya aina hiyo na utajikita kwenye mambo mbalimbali ikiwamo kuwa na vifaa vya uzimaji moto.

"Pia kusimamia ipasavyo sheria na taratibu za Mlima Kilimanjaro na kuandaa mpango wa kudhibiti moto kikamilifu unavyojitokeza kwa kushirikisha wadau mbalimbali, pia kuwekeza kwenye vifaa vya kubebea maji kwenye helikopta," alisema.

Alishukuru wadau mbalimbali na wananchi wanaozunguka mlima huo waliosaidia kuongeza nguvu ili kuzima moto huo na kusisitiza shughuli za utalii zinaendelea.

"Wadau ndani ya nchi waliosaidia ni pamoja na Kampuni ya watalii ya Zara na Altezza, Chama cha Mawakala wa Utalii Tanzania (TATO), vikosi vya Jeshi la Uhifadhi kutoka Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro, vikosi vya jeshi TANAPA na Jeshi la Zimamoto na tutatoa vyeti vya kupongeza mchango wao," alisema.

# Waitara: Nitamaliza mgawanyiko Tarime

**Na Ambrose Wantaigwa,** TARIME

MBUNGE mteule wa Jimbo la Tarime Vijijini, Mwita Waitara, ameahidi kuunganisha koo zote za jamii wilayani hapa ili kuboresha maisha ya wananchi.

Waitara alishinda kiti hicho kwenye uchaguzi mkuu mwaka huu katika jimbo ambalo miaka mitano iliyopita lilikuwa chini ya mbunge wa upinzani kupitia CHADEMA, John Heche.

Mbunge huyo alitoa ahadi hiyo katika mji wa mpakani wa Sirari wilayani Tarime wakati akiwashukuru wananchi wa eneo hilo kwa kumchagua kuwatumikia kwa miaka mitano ijayo.

Alisema ushindi wa CCM katika majimbo yote mawili wilayani hapa ni ishara kwamba wananchi wameongeza imani katika utendaji wa serikali ya awamu ya tano.

Waitara ambaye ni Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), alisema baadhi ya wanasiasa jimboni humo wamekuwa wakitumia siasa za kugawa wananchi kwa misingi ya koo, hivyo kusababisha mapigano ya mara kwa mara kati yao.

"Ushindi wa kishindo wa CCM katika majimbo yote ya Tarime Mjini na Vijijini yaliyokuwa upinzani ni ishara kwamba wananchi wamechoka na siasa za mgawanyiko na chuki miongoni mwa koo katika eneo hili," alidai Waitara.

Akizungumzia utekelezaji wa ilani ya chama chake cha CCM alisema katika miaka mitano ijayo, serikali iliahidi kupandisha hadhi ya mji wa Sirari kuwa mamlaka ya mji mdogo ili kusogeza huduma karibu na wananchi.

# Wanafunzi wapatiwa taulo za kike

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANAFUNZI wakike 30 wanaosoma Shule ya Msingi Ushirika na Sekondari ya Chamaguha katika Manispaa ya Shinyanga, wamepewa msaada wa taulo za kike, kwa ajili ya kuwahifadhi na hedhi kipindi cha masomo.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Aspire Products and Services (APS) ya jijini Dar es Salaam, Janeth Dutu, ambao wanajihusisha pia na masuala ya kijamii, alisema juzi kuwa wametoa msaada huo ili kumaliza utoro kwa wanafunzi wanapokuwa katika hedhi.

Alisema wametoa taulo za kike 400, kwa wanafunzi 10 kutoka Shule ya Msingi Ushirika na 20 kwa Sekondari ya Chamaguha, ambao hawana uwezo wa kununua taulo hizo, ili kuwastiri na hedhi na kuendelea na masomo katika mazingira rafiki. "Mimi nilisoma katika shule hii ya Msingi Ushirika, hivyo nafahamu adha ambayo wanaipata wanafunzi ambao hawana uwezo wa kuwa na taulo za kike kipindi wanapokuwa katika hedhi...taulo hizi zitakuwa msaada kwao na kutokatisha masomo wanapokuwa katika siku zao," alisema Dutu.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, ambaye alikuwa mgeni rasmi, alishukuru utolewaji wa taulo hizo, na kubainisha kuwa zitawastiri wanafunzi hao na hedhi kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Mmoja wa wanafunzi walionufaika na taulo hizo, Elizabeth Kagongoo, kutoka Shule ya Sekondari ya Chamaguha, alishukuru kwa niaba ya wenzake, na kueleza kuwa zitamsaidia.



Wachuuzi wa matunda wakisubiri wateja katika eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana. Papai moja liliuzwa kwa 2,000/-, wakati embe moja ni 1,000/-. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Diwani mteule akana kujiuzulu

**Na Said Hamdani,** LINDI

DIWANI mteule wa Kata ya Makonde, Jimbo la Lindi Mjini, Lunda Juma, wa Chama cha ACT-Wazalendo, amekanusha uvumi ulioenea mjini hapo kuwa amejiuzulu nafasi hiyo ambayo alipata baada ya kuwabwaga wagombea wengine katika uchaguzi uliofanyika Oktoba 28, 2020.

Lunda aliyepewa dhamana ya udiwani wa kata hiyo na wananchi wa Kata ya Makonde aliiambia gazeti hili kuwa hakuna kiongozi yeyote wa chama chake au yeyote mwingine aliyemshauri ajiuzulu nafasi hiyo, na kwamba taarifa hizo si za kweli.

Lunda alisema kuwa peke yake kwenye Baraza la Madiwani, hakumzuii kutekeleza majukumu aliyopewa ya kuwatumikia wananchi waliompa dhamana hiyo.

Diwani huyo mteule alisema taarifa za yeye kujiuzulu kabla ya kuapishwa ni uzushi unaoenezwa na wapinzani wake, na kwamba amekwishapigiwa simu nyingi sana na wengine kumtumia ujumbe mfupi kupitia simu yake ya mkononi wakitaka kujua juu ya madai hayo.

Alisema yeye amechaguliwa kwa kupigiwa kura na wananchi, hivyo hawezi kuwasaliti waliomchagua kwa hofu kwamba eti atakuwa peke yake kwenye Baraza la Madiwani.

Madai ya kujiuzulu kwa diwani huyo yamepingwa pia na mwenyekiti wa chama hicho, Isihaka Rashidi Mchinjita, ambaye alisema ofisi yake haijapokea taarifa yoyote, na kwamba chama kinatambua kuwa ndiye diwani halali aliyechaguliwa na wananchi.

# Mchungaji atoa somo baada ya uchaguzi

**Na Mohab Dominick,** KAHAMA

MCHUNGAJI wa Kanisa la FPCT, Mchungaji Kagoma, John Kasagamba, amewataka waumini wake pamoja na Watanzania kwa ujumla kuunga na Rais mteule, Dk. John Magufuli, na kuweka pembeni itikadi za vyama vyao kwa kuwa muda wa siasa umekwisha.

Mchungaji huyo amesema kwa sasa wananchi wanatamani kuona maendeleo kutoka kwa serikali waliyoichagua.

"Namshukuru Mungu kwa kutuvusha kipindi cha uchaguzi, uchaguzi umeisha, twende tukachape kazi, acha kuendelea kuhuzunika na kusononeka," alisema na kuendelea: "Huwezi kuyabadili matokeo, badala yake wahubiri wakahubiri injili na wafanyakazi wakafanye kazi na asiyefanya kazi na asile, kwa hiyo ninamshukuru Mungu kwa kutupatia viongozi watakaotupeleka ndani ya miaka 5."

Vilevile Kasagamba alisema kuwa Rais Magufuli ni kiongozi mwenye maono ya mbali, na kwamba amewaepusha Watanzania kukumbwa na gonjwa hatari la Covid-19 linalosababishwa na virusi vya Corona, ambalo linaendelea kutesa mataifa mbalimbali duniani.

Aidha, mchungaji Kagoma alisema kuwa Mungu alimwonyesha Rais Magufuli maono ya kumwambia waambie watu wake wafunge na kuomba kwa muda wa siku tatu kwa dini zote, hata wale ambao hawana dini ili kulikomboa taifa lake kwa ugonjwa huo hatari.

Mchungaji huyo aliyasema hayo wakati wa ufunguzi wa mkutano wa Injili unaolenga kusambaza neno la Mungu unaofanyika katika viwanja vya soko la wakulima na utahitimishwa Jumapili.



Wanachama wa Umoja wa Wanaharakati Wazalendo na Siasa Tanzania (UWAST), wakionyesha alama inayoashiria amani, wakati wa mkutano na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam juzi, kuhusu kulinda amani ya nchi. Wa (pili kulia) ni kiongozi wa umoja huo, Kunje Ngombale Mwiru na wanachama Amina Ahungu (kulia), Popadick Mbonea (wa pili kushoto) na Feruzi Abeid. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wakuu wa vyuo waafiki mpango ufadhili masomo

**Na Elizabeth Zaya**

WAKUU wa vyuo vya kilimo vinavyonufaika na mpango wa ufadhili wa masomo maarufu kama kilimo viwanda scholarship programu, wameupongeza mpango huo unaowasaidia wanafunzi wanaotoka katika familia maskini.

Kilimo viwanda, ni mpango ulioanzishwa na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) wenye nia ya kusaidia kuongeza wataalamu wa kilimo nchini, huku ukiwalenga wanafunzi wanaotoka katika familia zenye vipato duni.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa awamu ya pili ya mpango huo uliofanyika jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Chuo cha Kaole Wazazi College of Agriculture kilichopo Bagamoyo mkoani Pwani, Sinani Simba, alisema mpango huo umeweza kuwasaidia wanafunzi ambao kama usingekuwapo wasingepata nafasi ya kusoma na kutimiza malengo yao ya kimaisha.

"Napenda kuwapongeza SBL kwa kuwajali wanafunzi wanaotoka familia maskini, pasipo msaada unaotokana na mpango huu, ni wazi kuwa wasingeweza kusoma na kutimiza ndoto zao za kimaisha," alisema.

Mkuu wa Chuo cha Kilacha Agricultural and Livestock Training Center kilichopo Moshi mkoani Kilimanjaro, Benito Mwenda, alisema pamoja na kuwasaidia wanafunzi wanaotoka katika familia maskini, mpango huo pia unasaidia kuzalisha wataalamu wa kilimo ambao ni muhimu katika maendeleo ya kilimo nchini.

"Kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wetu na kwa namna ya pekee napenda kuipongeza SBL kwa kuona umuhimu wa kusaidia maendelea ya sekta hii nyeti.

"Mpango huu watasaidia sana kuongeza idadi ya wataalamu watakaokuwa wanafanya kazi na wakulima ili kuwashauri namna bora ya kuongeza tija na uzalishaji katika shughuli zao za kilimo."

Kupitia mpango wa kilimo viwanda jumla ya wanafunzi 40 wamenufaika na ufadhili wa masomo kwa mwaka wa fedha 2019/2020, huku wengine 30 wakitarajia kunufaika katika mwaka 2020/2021.

Mkurugenzi Mtendaji wa SBL, Mark Ocitti, alisema, mpango wa kutoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa kilimo unalenga kuisaidia serikali kuwajengea uwezo wa kuzalisha zaidi wakulima kupitia wataalamu wa kilimo ambao watawasaidia na kuwashauri.

Alifafanua kuwa wametenga Sh. milioni 120 ambazo zitatumika kila mwaka kwa ajili kuwalipia wanafunzi wenye sifa na ambao lengo lao ni kusoma masomo ya kilimo na kuongeza kuwa wanufaika watatoka katika familia za wakulima zenye kipato cha chini.

"Ili kutekeleza mpango huu, tunashirikiana na vyuo vinne vya ndani ambavyo vinafundisha masomo ya kilimo. Tunaamini mpango huu utasaidia kuongeza idadi ya wataalamu wa kilimo nchini, ambao ni nguzo muhimu ya kuwasaidia wakulima kuongeza uzalishaji wao na mwisho wa vipato vyao," alisema.

Alisema vyuo ambavyo kampuni hiyo inashirikiana navyo katika utekelezaji wa programu hiyo ni Kaole Wazazi College of Agriculture kilichopo Bagamoyo mkoani Pwani, Kilacha Agriculture and Livestock Training Center kilichopo Moshi, Mt. Maria Goretti College of Agriculture cha Iringa na Igabiro Training Institute of Agriculture kilichopo Bukoba, mkoani Kagera.

## Wapewa jukumu kusimamia ubora wa zao la korosho

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

OFISA Ushirika wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, Juma Chaka, amewataka viongozi wa vyama vya msingi (AMCOS) kuhakikisha wanasimamia kwa weledi zao la korosho, ili lihifadhiwe katika magunia likiwa na ubora.

Chaka amewataka viongozi hao wa AMCOS Mkuranga kutekeleza agizo la Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evalist Ndikilo, ambaye aliwataka viongozi hao kuhakikisha ubora wa korosho unakuwapo kabla ya kuwekwa katika magunia.

"Mtekeleze maagizo ya Mkuu wa Mkoa kwa kuhakikisha viongozi wa AMCOS mnasimamia zao la korosho kabla ya kuwekwa kwenye magunia, ili zinapoingizwa katika maghala kusiwe na kasoro," alisema.

Chaka aliyasema hayo baada ya kukamilika kwa uchaguzi wa mwenyekiti wa AMCOS Wilaya ya Mkuranga, ambapo Shabani Penda, alichaguliwa kwa kupata kura 27 na Abdallah Athumani alichaguliwa kuwa makamu mwenyekiti kwa kupata kura 12. Pia, ofisa ushirika huyo aliwataja wanachama Rajabu Kihegero na Abdallah Maulidi, ambao walichaguliwa kuziba nafasi zilizopungua za ujumbe wa bodi.

Mjumbe wa Bodi ya AMCOS, Omary Maluyo, alimpongeza ofisa ushirika huyo kwa kuwa karibu na vyama, huku akiziomba taasisi za kifedha kuweka riba nafuu ikiwamo masharti yanayotekelezeka ili wakulima wavutiwe kukopa.

Mwenyekiti aliyechaguliwa, aliwaomba wanachama wawape ushirikiano ili kufanikisha kuwapo na maendeleo katika chama, huku aliwataka wajiandae kwa mkutano mkuu ujao wa uchaguzi.

# Hofu ya tembo yabadili ratiba ya masomo

**Na Asraji Mvungi,** MWANGA

SIKU moja baada ya mwalimu wa Shule ya Sekondari ya Kwangu wilayani Mwanga, Mkoa wa Kilimanjaro, kuuawa na tembo, uongozi wa shule hiyo umefanya mabadiliko ya muda wa kuanza na kumaliza masomo.

Akizungumza na Nipashe iliyotembelea shule hiyo, Makamu Mkuu wa Shule hiyo, David Mwingira, alisema kutokana na tishio la tembo, wanalazimika kuchelewa kuanza masomo, ili kuwasubiri wanafunzi ambao wanachelewa kufika shuleni.

Alisema hatua ya wanafunzi kuchelewa kuja shuleni inalenga kukwepa tembo hao ambao wakati wa asubuhi wanakuwa wanazagaa mitaani.

"Kwa sasa masomo yanaendelea kama kawaida, lakini tunalazimika kuchelewa kuanza ili wale wanafunzi wanaokaa nyumbani wafike na kumaliza mapema ili wawahi kufika nyumbani kabla ya giza. Naye mwalimu wa taaluma wa shule hiyo, alisema wameanza kutoa elimu ya saikolojia kwa wanafunzi inayolenga kuwaondolea hofu inayopatikana na tembo hao ambayo imeongezeka baada ya mwalimu wao kuuawa.

"Japokuwa masomo yanaendelea, lakini wanafunzi na hata sisi walimu tumeingiwa na hofu kwani makundi ya wanyama hawa kila siku yanasogea karibu, sasa hivi sisi hatutembei usiku, wapo wengi na wengine wana watoto, kwa hiyo tunajitahidi, lakini kwa kweli hali sio shwari," alisema.

Akizungumza kwa njia ya simu Kamanda wa Kikosi cha Kuzuia Ujangili Kanda ya Kaskazini (KDU), Emanuel Nnko, alikiri kuongezeka kwa makundi ya tembo katika eneo hilo, ingawa wanaendelea kuyakabili.

"Hata juzi baada ya lile kundi kuua, usiku wa manane walirudi katika eneo lile, ingawa tulifanikiwa kuwafukuza, lakini kiukweli tatizo ni kubwa," alisema Nnko.

Nnko alisema wanakesha usiku kufukuzana na tembo na amewaomba wananchi kuendelea kutoa ushirikiano.

## Tanzania bado inaitembelea nyota ya Tume ya Jaji Nyalali ?




Ukurasa 12



Ukurasa 14

**HUSSEIN ALI MWINYI**

**siasa**

JUMATANO NOVEMBA 4, 2020

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

# WAPIGAKURA KIDUCHU 2020

## ■Utafiti wa kina uje na jibu kwanini kudorora upigaji kura kila msimu?

**Na Sabato Kasika**

UCHAGUZI mkuu wa Oktoba 2020 umehitimishwa wiki iliyopita ukiwa na mengi ya kusimulia, lakini kubwa zaidi ni idadi ndogo ya wapigakura waliojitokeza kuchagua rais, wabunge na madiwani makala ikitazama rejista na takwimu za Tanzania Bara.

Idadi ya waliojiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura kwa mujibu wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ni milioni 29.19, lakini waliojitokeza kupigakura ni milioni 15, wengine milioni 14 hawakuonekana vituoni, licha ya kwamba ilikuwa siku ya mapumziko na vituo vilifunguliwa siku nzima.

Kuendelea kupungua kwa idadi ya wapigakura ni jambo ambalo wadau wakiwamo vyama vya siasa NEC, wagombea, wasomi vyuo vikuu na watafiti kukaa pamoja na kutafakari kwa kina ili kuja na majibu ambayo yanayoweza kuwa ni ufumbuzi wa kudumu wa mazoea ya kukimbia kupiga kura.

Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, serikali, asasi za kiraia na wananchi nao ni sehemu ya watu ambao wanatakiwa suala la umma kuacha kupiga kura liwafikirishe zaidi na kulipatia ufumbuzi.

Kumbukumbu zinaonyeha kuwa, katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, wapigakura walioandikishwa walikuwa ni milioni 23.161, lakini waliopiga kura walikuwa ni milioni 15. 589 pekee.

Ilikuwa ni baada ya uchaguzi wa mwaka huo, ndipo aliyekuwa Mwenyekiti wa NEC, Jaji Mstaafu, Jaji Damiani Lubuva, anatoa idadi hiyo ya wapigakura ambayo ilikuwa ni ndogo ikilinganishwa na matarajio.

Badala ya wanaopiga kura kuongezeka, imekuwa kinyume kutokana na kuzidi kupungua katika uchaguzi wa mwaka huu kama ilivyotangazwa mwenyekiti wa NEC, Jaji Mstaafu wa Mahakama ya Rufaa, Semistocles Kaijage.

Wakati mwingine ilidhaniwa kuwa huenda kutenga siku ya Jumapili kuwa ya kupiga kura ilikuwa ni sababu mojawapo ya kuwafanya baadhi ya wananchi wasijitokeze kushiriki uchaguzi, kwa sababu wanakuwa kwenye ibada.



Wakazi wa jijini Dar es Salaam wakiwa kwenye foleni ya kupiga kura katika uchaguzi mkuu uliofanyika wiki iliyopita. **PICHA: MIRAJI MSALA**

Mwaka huu, NEC ilibadili mfumo na kwa mara ya kwanza uchaguzi ukafanyika katikati ya wiki, Jumatano Oktoba 28 , hata hivyo matokeo yake watu wengi zaidi hawakujitokeza.

**TATIZO NI NINI?**

Awali ilidhaniwa kuwa wengi walitamani kumiliki kitambulisho cha kura chenye mfumo wa bayometria ili kuwarahisishia kupata huduma kwenye benki hasa kufungua akaunti na kitambulisho cha usajili wa simu kadi.

Hata hivyo, Watanzania wana vitambulisho vya taifa ambavyo vina taarifa za bayometria (alama za vidole), hivyo inaonekana pengine kunahitajika utafiti zaidi kuzijua sababu za kudorora kupigakura.

Kuna sababu mbalimbali, ambazo zinatajwa kuchangia kuwapo kwa idadi ndogo ya wapigakura, ikiwamo suala la kuichumi, kwamba mtu anaona ni bora akatafute riziki kuliko kwenda kupiga kura.

Wapo wanaoamini kwamba, kwenda kupiga kura ni sawa na kuwatafutia wengine ulaji na maisha bora huku wao hali zao zikiendelea kuwa duni, hivyo wanaamua kukaa nyumbani ama kwenda katika shughuli nyingine.

Aidha, wengine waamini kuwa, kupiga kura ni sawa na kujisumbua ama kupoteza muda, kwa madai kwamba, wanaotangazwa kushinda wanafahamika, pengine si chaguo lao.

"Kwa nini nipoteze muda wangu kwenda kupigakura wakati inajulikana wazi kuwa mshindi ni kutoka chama fulani? Siwezi kupoteza muda wangu, kama sina la kufanya bora nikae nyumbani tu," anasema Winifrida Elias.

Mkazi huyo wa Kimara Dar es Salaam, anasema, hawezi kukaa katika kituo cha kupigia kura siku nzima na kupoteza muda kwa jambo ambalo anajua kuwa mwisho wake matokeo yanakuwaje.

Hizo ni sababu ambazo sehemu kubwa ya wasiopiga kura huwa wanazitoa, lakini watu kama hao bado wanahitaji kuelimishwa waone umuhimu wa kushiriki katika uchaguzi.

Wananchi hao wanatakiwa kukumbushwa kuwa kura moja inaweza kubadili matokeo ya uchaguzi, hivyo waachane na mawazo hayo ili wawe wanajitokeza kwa wingi kuchagua viongozi wanaowataka kwani ni haki yao kidemokrasia.

**ELIMU YA MPIGAKURA**

Ili kuwahamasisha watu kupigakura wanahitaji elimu ya mpigakura ambayo ni nyenzo na kielelezo muhimu katika kumwezesha kila mwananchi kuelewa mchakato wa uchaguzi na nafasi yake katika kuchagua viongozi.

Elimu hiyo huwajengea uelewa wananchi kuhusu haki na wajibu wao kushiriki katika mchakato wa uchaguzi wakiwa na taarifa kamili na sahihi juu ya michakato yote ya uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani.

Vilevile elimu ya mpigakura hutolewa kwa wananchi wote kwa lengo la kuwawezesha kuelewa kuhusu sheria, kanuni, taratibu za mchakato mzima wa uchaguzi, wajibu wao na umuhimu wa kushiriki katika uchaguzi.

Elimu hiyo inatakiwa isiwe na hisia, ubaguzi wala itikadi za kisiasa na inalenga kuwahamasisha wananchi kutumia haki yao ya kikatiba kuchagua viongozi watakaowaongoza, ili kujenga demokrasia na utawala bora nchini.

Kwa hali kama hiyo wananchi wanapoipata, wanahamasika na wanakuwa tayari kwa hiari na ufahamu wao na kwa kujiamini kushiriki katika mchakato wa uchaguzi wakiwa na mtazamo wa kukuza demokrasia.

Hivyo, dhana ya elimu ya mpigakura inahusisha pia usambazaji wa taarifa, vielelezo na vipindi mbalimbali katika vyombo vya habari kwa lengo la kuelimisha wananchi juu ya mchakato wa uchaguzi.

Vilevile mchakato huo mzima, unahusisha uandikishaji wa wapigakura, ugawaji wa majimbo, uwekaji wazi daftari, kampeni, utaratibu wa kupiga kura na vituo vya kupigia kura.

**UMMA UMEELIMISHWA?**

Jumla ya asasi 245 za kiraia zilipewa vibali vya kutoa elimu ya mpigakura wakati wa uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura, ulionza Julai mwaka jana na nyingine 97 zilipewa vibali vya uangalizi wa uchaguzi mkuu.

Julai mwaka jana, Mkurugenzi wa NEC, Dk. Wilson Charles Mahera, alitangaza kwamba asasi hizo zinatakiwa kutoa elimu hiyo kote nchini.

Kwa upande wake mwenyekiti wa NEC Jaji Kaijage, alisema, kulingana na sheria ya uchaguzi ya 2004 , kifungu cha 4C, NEC imepewa mamlaka ya kutoa elimu ya mpigakura nchi nzima, kusimamia na kuratibu taasisi au ssasi zenye sifa ya kutoa elimu hiyo.

Anafafanua kuwa mwaka 2010 tume hiyo iliwapa vibali vya kutoa elimu ya mpigakura kwa asasi za kiraia 66, wakati mwaka 2015, zilikuwa 447na mwaka huu zilikuwa 245.

Anasema, njia zilizotumika kufikisha elimu hiyo ni kukutana na wananchi ana kwa ana, kushiriki maonyesho mbalimbali, mikusanyiko ya kijamii, kutumia gari la tangazo la NEC, vyombo vya habari na machapisho yakiwamo mabango.

### USHINDI HUU WA CCM

# Tanzania bado inaitembelea nyota ya Tume ya Jaji Nyalali ?



Rais Mteule John Magufuli, baada ya kukabidhiwa cheti cha ushindi wa uchaguzi wa urais 2020 na Tume ya Taifa ya Uchaguzi . Alipata ushindi wa asilimia 84.4. **PICHA: IKULU.**

**Na Mwandishi Wetu**

MAPEMA mwaka 1992 taifa liliingia kwenye mfumo wa vyama vingi vya siasa na uchaguzi mkuu wa kwanza ulifanyika mwaka 1995 kukiwa na mchuano mkali baina ya mgombea wa CCM Benjamin Mkapa na Augustine Mrema wa NCCR Mageuzi, wakigombea kiti cha urais.

Kwa upande wa Zanzibar alikuwa Dk. Salim Amour wa CCM na Seif Sharifu Hamad wa CUF walichuana kwenye urais wa Zanzibar, mfumo huo wa vyama vingi unaelezwa kuwa haukukubalika.

Muasisi wake ni Rais Ali Hassan Mwinyi, aliyeunda tume ya kuangalia mambo mbalimbali likiwamo suala la mfumo bora wa siasa badala ya chama kimoja, hali ya Muungano na sheria kandamizi.

Tume hiyo ikiwa chini ya Jaji Mkuu wa wakati huo, Francis Nyalali, ilizunguka nchi nzima na kukusanya maoni ya wananchi na lilipokuja suala la kufanya marekebisho ya katiba na kuachana na mfumo wa chama kimoja cha siasa ili kuingia kwenye utaratibu wa vyama vingi vya siasa, hilo halikukubalika.

Watanzania wengi hawakukubaliana na pendekezo hilo na uwepo wa vyama vingi haukuwa ridhaa yao kwa vile asilimia 80 ilivikataa na waliokubali kuwa na mfumo huo walikuwa asilimia 20 pekee.

Lakini busara za viongozi akiwamo Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, wakashauri kuwa Tanzania iingie kwenye vyama vingi na kwamba utaratibu wa wachache badala ya wengi wape ulichukua mkondo wake.

Ni kwa sababu hao waliokubali mageuzi licha ya kuwa kiasi kidogo cha asilimia 20, walionekana kuwa wataongezeka na kuwa wengi zaidi miaka inavyokwenda.

Uamuzi huo ulifanyika kwa kuangalia upepo wa mageuzi uliovuma sehemu mbalimbali duniani na wakati huo dola la Jamhuri za Kisovieti la USSR(Urusi) lililokuwa linaunga mkono mrengo wa ujamaa lilikuwa limesambaratika na kufungua milango ya mageuzi ya kisiasa na kiuchumi ili kupanua demokrasia zaidi.

Kwa mantiki hiyo, huenda Watanzania wanaendelea kutembelea nyota ya chama kimoja na hawajawa tayari kwa mfumo wa vingi kama ilivyotokea kwenye uchaguzi mkuu wa wiki iliyopita.

Watanzania wengi wameichagua CCM kwa zaidi ya asilimia 90 kwa vile kwa Tanzania Bara yako majimbo 214 wakati Zanzibar na Pemba ni 50.

Kwa mujibu wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kwa Tanzania Bara wapinzani karibu wote walipoteza majimbo isipokuwa wawili pekee Shamsia Mtamba CUF aliyeibuka kidedea Mtwara Vijijini na Aida Khenan (Chadema) aliyepata ushindi Nkasi Kaskazini mkoani Rukwa.

Kwa upande wa Zanzibar wapinzani wakuu wa CCM ambao ni CUF na ACT -Wazalendo , hawakufanikiwa kupata ushindi wa kishindo hata kwenye ngome zao kongwe.

> Uchaguzi huo si kwamba umeweka rekodi ya kutembelea nyota ya chama kimoja kama ambavyo ilishuhudiwa na Tume ya Nyalali, lakini pia unatoa fursa ya kutafakari zaidi kuwa ile hofu ya wachache wape maana huenda wakaongezeka haikuwa na mashiko.

Kwa hali hiyo huenda bado fikra za kuwa na chama kimoja zipo kwenye hisia za Watanzania wengi ndiyo maana uchaguzi mkuu umeshuhudia Bunge la Jumhuri ya Muungano pamoja na Baraza la Wawakilishi likiwa la CCM au la kijani.

Uchaguzi huo si kwamba umeweka rekodi ya kutembelea nyota ya chama kimoja kama ambavyo ilishuhudiwa na Tume ya Nyalali, lakini pia unatoa fursa ya kutafakari zaidi kuwa ile hofu ya wachache wape maana huenda wakaongezeka haikuwa na mashiko.

Kwa mujibu wa NEC, idadi kubwa ya waliojiandikisha kupiga kura mwaka huu ni vijana, hivyo nao wameanza kuona umuhimu wa kubaki na chama kimoja badala ya kuwa na utitiri wa vyama vingi?

Lakini huenda suala si kutembelea nyota ya mwaka 1992 ya asilimia 80 ya kutaka kuiona Tanzania ikibaki na chama kimoja badala yake ni huenda wanaotaka mageuzi hawajitokezi kupigakura.

Huenda wanabaki kuwa wanasiasa za ushabiki na za majukwaani lakini si wa kushiriki kwenye kuwachagua viongozi kwenye sanduku la kupigia kura.

Kwa mtizamo mwingine inaweza kuonekana kuwa vyama vya siasa hasa vya upinzani havina wanachama. CCM inabakia kuwa na mtaji mkubwa wa wanachama ambao mbali na kukiunga mkono chama chao, wanakipigia kura, wanashiriki kampeni na wanafahamu wanachokifanya.

Tofauti na hali ilivyo kwenye washindani wao, wapinzani wanabakia kuwa watazamaji, wahamasishaji wakati wa kampeni lakini waoga na pengine wanachama ambao hawajafanya uamuzi wakati wa kupigakura na kusema wanakwenda kumpa nani kura zao.

Hata hivyo, pengine kwa vile serikali ilivyozuia vyama vya siasa kushiriki harakati za kisiasa kwa miaka mitano, wanachama hao hawakuwa na mwamko wala hamasa ya kisiasa.

Watanzania kuusimamia mfumo wa chama kimoja ni changamoto kwa vyama vya ushindani kujiangalia upya na kuwauliza wanachama wao wanataka nini? Wangependa wapinzani wafanye jambo gani kuboresha siasa za ushindani nchini kwa vile inavyoelekea kile kinachofanyika au kilichofanyika kwa miaka 25 ambayo uchaguzi wa vyama vingi umefanyika hakijawaridhisha.

Vuguvugu la kisiasa lililoanza mwaka 995 lilishuhudia mchuano mkali kati ya Mkapa na Mrema, lakini ushindani uliongezeka zaidi 2015 baina ya Rais John Magufuli wa CCM alipochuana na Edward Lowassa wa CHADEMA.

Hata hivyo, uchaguzi na ushindi si mwisho wa maisha kila upande ujizatiti kulinda amani, kutenda haki na kuipeleka Tanzania ikiwa salama, yenye amani, utulivu na furaha kwenye uchaguzi mkuu wa Oktoba, 2025.

# CCM kampeni hazikuwa kuomba ridhaa ila kueleweka mwishoni



Rais John Magufuli, akipiga kampeni za kutangaza makubwa yaliyofanywa na awamu ya tano. **PICHA: IKULU.**

**Na Ani Jozeni**

BAADHI ya taasisi waangalizi wa uchaguzi waliohusika na kufuatilia upigaji kura wameonyesha mshangao wa jinsi hatua za mwisho za uchaguzi zilivyokwenda, ingawa hapakuwa na jambo la kushangaza kwani walishapewa taarifa mapema ya hali ya haki za binadamu nchini.

Ni taarifa ambayo serikali iliiangalia kwa makini kiasi na kutoa majibu ya jumla, kwamba lawama kuhusu rushwa za mwaka 2015 sasa hazipo na badala yake zipo za kutoheshimiwa ipasavyo haki za binadamu.

Waziri wa Mambo ya Nje, Profesa Palamagamba Kabudi, hakuhitaji kujibu kwa undani, akijua sifa za Rais John Magufuli zinatosha. Kuhama makada upinzani walioguswa na mwelekeo wake kulishatosha kuonyesha ridhaa halisi iliyopo.

Hali hiyo kimsingi itabakia hivyo kuhusu mwenendo wa uchaguzi mkuu, ambao waangalizi wa taasisi moja ya Umoja wa Afrika kwa Ukanda wa Kusini mwa Afrika (EISA) inasema ulikuwa na viwango hafifu vya demokrasia ukilinganisha na wa 2015.

Kwa hisia ya taarifa hiyo na mustakabali wa kuangalia mwenendo wa uchaguzi kwa jumla, tathmini hiyo inawezekana ikawa ni karipio kwa utawala wa awamu ya tano, kuwa viwango vya demokrasia vimepungua.

Ni kweli, lakini inabidi kuonisha na jibu la Waziri Kabudi, kuhusu suala hilo, kwani uchaguzi wa 2015 ulikuwa pia ni kilele cha vielelezo vya rushwa, kuwezesha uvutano.

Mvutano wa kidemokrasia ni hali ambayo wananchi wanaombwa kutoa ridhaa kuhusu nini kifanyike katika miaka mitano inayofuata, kati ya dhamira ya kundi lililoko madarakani na wanaopingana nalo.

Ni mazingira ambako hakuna uamuzi wa dhati yaliyopo kuhusu nini kifanyike, hivyo kila upande unaomba ridhaa kuwa unachotaka kufanya ni bora zaidi kwa mustakabali wa nchi kuliko washindani wao.

Yako pia mazingira ya uchaguzi ambako kinachotakiwa kufanyika tayari kinajulikana na hakipo mezani kujua ni nini au kinaongozwa na nani ila yako maeneo ushindani unawezekana kwa wagombea tofauti.

Ndiyo hulka iliyokuwa inatawala chaguzi wa chama kimoja, 1965 hadi 1990, kuwa katika kutafuta nani awe mbunge kuwe na ushindani wa watiania wawili wa chama hicho hicho, ila katika nafasi ya urais wananchi 'waelekezwe' nani anafaa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa maana hiyo alikuwa anatafuta uthibitisho wa kukubalika kwa jambo hilo kwa kura za 'ndiyo' na 'hapana,' kwani wale wasio na utashi halisi wa kumuunga mkono wangebaki nyumbani na wanaomshangilia watoke kumpa kura. Siyo uchaguzi huru na haki lakini akiwa anachukiwa watajazana kupita kura atoke na watajua hilo.

Pamoja na kupitisha uamuzi wa kuingia kwenye mfumo wa vyama vingi mwaka 1992 na uchaguzi mkuu wa kwanza kwa mfumo huo 1995, bado kimsingi kuna chembe ya mfumo wa chama kimoja iliyobaki.

Kwa mfano kabla ya kufanyika kwa uchaguzi mkuu mwaka huu, shughuli mojawapo muhimu ilikuwa ni kumbukumbu ya miaka 21 ya kifo cha Mwalimu Julius Nyerere na mgeni wa heshima katika kumbukizi hizo huwa ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Mwalimu Nyerere Foundation, Joseph Butiku, aliyekuwa msaidizi wake wa karibu kwa miaka mingi.

> Kwa maana hiyo kuna misukumo na mabadiliko ndani ya CCM na katika hulka pana zaidi kuhusu sera na kuhusu demokrasia, ambayo ilikuwa mezani katika uchaguzi mkuu, kwa maana kuwa hapakuwa na haja ya kutoa nafasi pana ya kuvuruga kinachofanywa na serikali, kwa kisingizio cha kanuni za kimataifa.

Pia anaongoza kundi lisilo rasmi katika CCM wanakotokea baadhi ya makada waandamizi waliojumuika huko wakati wa vita (kiini macho) dhidi ya ufisadi nyakati za awamu ya nne.

Ni makada ambao walisemekana kuukaribia zaidi uongozi wa CCM na mgombea wake wa urais wakati waziri mkuu wa kwanza wa awamu hiyo alipoona amedhulumiwa, akahamia upinzani kundi la Butiku likaamini kuwa 'CCM imejisafisha.'

Ni hisia kuwa kulikuwa na kada mmoja au wawili wenye mwelekeo wa 'ubepari' kwa upande mmoja na 'ufisadi' kwa upande mwingine, hisia ambayo haikuwa sahihi na ni eneo mojawapo la kuunda makundi ndani ya chama tawala na kutafuta mbeleko za kiitikadi, nani mwema (apendekezwe) na nani 'fisadi' akae pembeni. Aliyepitishwa 2015 alipoanza kuwasaka wala rushwa halisi na wabadhirifu (mafisadi) serikalini, wadau wa kampeni potofu ya awali hawakuwa na la kusema, wakahamia mitandao ya kijamii, wakiwa na 'kigogo' akiongoza shutuma, akaingia upinzani, akapewa bendera, akakwama. Kampeni ya CCM ilikumbushia kazi iliyofanyika, kwamba iendelee kwa miaka mitano.

Kwa maana hiyo kuna misukumo na mabadiliko ndani ya CCM na katika hulka pana zaidi kuhusu sera na kuhusu demokrasia, ambayo ilikuwa mezani katika uchaguzi mkuu, kwa maana kuwa hapakuwa na haja ya kutoa nafasi pana ya kuvuruga kinachofanywa na serikali, kwa kisingizio cha kanuni za kimataifa.

Kwa mfano aliyekuwa mshindani tangulizi wa mgombea anayetaka ridhaa muhula wa pili alikuwa ni mpinzani ambaye hakuwahi kuelewa umuhimu wa vita ya kuikomboa Tanzania kiuchumi, vita ya madini akiiponda katika kila nafasi aliyopata bungeni na nje ya bunge. Endapo vita hiyo ingekuwa ni suala tu la mwelekeo wa sera lingekuwa jambo moja, lakini anayeifahamu Tanzania anajua lina utukufu kiasi gani.

Anasema Rais Nyerere akitembelea Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Agosti 1978, akazungumza katika hadhara ukumbi wa Nkrumah, akajibu swali kuhusu kufutwa kwa serikali huru ya wanafunzi, baada ya maandamano yaliyokatazwa, ukawekwa Umoja wa Vijana CCM badala yake.

Alisema (baada ya maelezo ya awali) 'every country has a government it deserves,' (kila nchi ina serikali inayoistahili). Hapawezi kuwa na mageuzi ya kina katika kila eneo la udanganyifu na ukosefu wa uwajibikaji, halafu wale wanaodharau kazi hiyo wapewe nafasi ya kuibeza na kuikweka pembeni katikati ya kipindi halisi cha kikatiba kilichopo, mihula miwili. Ni kweli wanayosema waangalizi hao kuwa uchaguzi mkuu 2015 ulikuwa na viwango bora zaidi vya kidemokrasia ila ni kwa sababu hapakuwa na 'jema' linalolindwa.

# HUSSEIN ALI MWINYI

## •Tunda la kizazi kipya, nuru na matumaini Z'bar
## •Rais wa kwanza aliyezaliwa baada ya Mapinduzi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

RAIS mpya wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ni Dk.Hussein Ali Mwinyi, aliyekula kiapo juzi na kutinga ikulu akiwa rais wa nane wa Zanzibar tangu visiwa hivyo kupata uhuru 1964.

Ana sifa pekee akiwa ni Rais wa Zanzibar aliyezaliwa baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964 yaliyomng'oa Sultan Jamshid bin Abdullah Al Said na kumaliza utawala wa Kiarabu visiwani hapo.

Mwinyi aliyezaliwa Desemba 23, 1966 na hivyo kutafsiriwa kuwa ni kiongozi wa kizazi kipya chenye nuru ya matumaini kwa wananchi wa Zanzibar wa sasa ambao wengi ni vijana.

Katika uchaguzi mkuu wa Octoba 28, mwaka huu Dk Mwinyi, anaibuka kidedea akipata kura 380,402 sawa na asilimia 76.27 na kuwabwaga wapinzani wake akiwamo mwanasiasa maarufu na mkongwe Visiwani Zanzibar Maalim Seif Sharif Hamad aliyepata kura 99,103 sawa na asilimia 19.87.

Baada ya kutangazwa na Tume ya Uchaguzi Zanzibar kuwa mshindi hatua iliyofuatia ni kula kiapo na kukabidhiwa rasmi madaraka ya kuongoza Zanzibar.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akijiandaa kuanza kazi kwa kula kiapo cha utii, uaminifu na utumishi kwa wananchi. **PICHA: IKULU ZANZIBAR.**

**ANAPOKULA KIAPO**

"Mimi Hussein Ali Mwinyi naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu kwamba nitakuwa mwaminifu kwa Zanzibar na kuitumikia kwa moyo wangu wote na kwamba nitaihifadhi, nitailinda na kuitetea katiba ya Zanzibar na ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania na watu wake kwa mujibu wa sheria iliyowekwa na kuomba Mwenyezi Mungu unisaidie", anasema na kuahidi Dk. Mwinyi.

Anaahidi katika kiapo kuwa mwaminifu na mtumishi wa Wazanzibari na Watanzania na kuendelea kuongeza katika kiapo chake hicho:

"Mimi Hussein Ali Mwinyi naapa kwamba nitatekeleza kazi zangu za urais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uadilifu na kutimiza wajibu wangu kwa moyo mkunjufu na kwamba nitawatendea haki watu wote kwa mujibu wa katiba na sheria na nikiongozwa na haki, mila na desturi ya Zanzibar bila ya kushawishiwa,woga wala chuki....".

Kumalizika kwa kiapo hicho kuliamsha shangwe na vigelele kwa mamia ya wananchi waliohudhuria sherehe hizo ambazo zilihudhuriwa na wananchi wa mikoa tano ya Zanzibar -Unguja na Pemba.

**ANAPOIPELEKA ZANZIBAR**

Mwelekeo wa serikali atakayoiongoza baada ya kula kiapo mbele ya Wazanzibari na viongozi mbalimbali wa Serikali ya Zanzibar na Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk Mwinyi anaahidi kuwa ataongoza serikali yake kwa kusimamia misingi ya haki,uwakibikaji na usawa katika kuwatumikia wananchi.

"Nitaunda serikali yenye misingi ya kulinda haki, uwajibikaji na usawa tena nitaongoza bila ya kumbagua mtu anapotoka, itikadi ya chama au dini, nitaweka usawa kwa watu wote'" anasema Dk Mwinyi baada ya kula kiapo.

Anawaambia mashuhuda wanaomsikiliza wakiwamo wanaomtizama mubashara kuwa atahakikisha anaendeleza pale alipoishia Rais Mstaafu Dk Ali Mohamed Shein na kumshukuru kwa hekima zake na busara alizozitumia wakati wote tangu alipoteuliwa kushika wadhifa huo.

Rais huyo mpya wa awamu ya nane ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, anasema kwamba atashirikiana na viongozi na wananchi, katika kuleta maendeleo ya Zanzibar na kuwataka Wazanzibari kudumisha amani na umoja wa kitaifa ili kufikia malengo ya maendeleo pamoja na kuleta mapinduzi ya uchumi wa Zanzibar.

"Nakusudia kuunda serikali makini yenye utendaji kazi bora, yenye kuwajibika kwa wananchi na kuchagua viongozi waadilifu ili kufikia malengo ya kuleta maendeleo ya haraka kwa Wazanzibari." Anaahidi Rais Mwinyi.

**SERIKALI INAYOWAJIBIKA**

Anachosisitiza ni kuunda serikali yenye uwezo wa kujenga misingi ya uwajibikaji yenye kupiga vita ubadhilifu ili kuharakisha maendeleo ya Zanzibar.

Anataka kuwa na serikali inayoondoa kero zinazowagusa wananchi kwa kuhakikisha viongozi wanashuka kushughulikia matatizo ya wananchi.

Anasema anataka kuona kila mtu anafaidika na rasilimali zinazopatikana nchini na kwamba serikali yake mpya itazingatia usawa na uwezo wa mtu kufanya kazi bila ya kuangalia mtu anatoka wapi.

"Naahidi kuunda serikali makini yenye uadilifu itakayoleta kasi ya maendeleo na kuwatumikia wananchi wote kwa usawa bila ya kujali wapi mtu anatoka"alisema.

KUSHIRIKIANA NA WENZAKE

Rais Dk Mwinyi anasema uchaguzi umekwisha na sasa kazi kubwa iliyopo mbele yake na ya Wazanzibari ni kuijenga Zanzibar yenye matumaini kwa kushirikiana na makundi mbali ikiwamo vyama vya siasa.

Anasema yupo tayari kushirikiana na vyama vyengine vya siasa kuijenga Zanzibar mpya yenye matumaini na kwamba huo ndiyo wakati wa kushirikiana na kuweka pembeni tofauti za kisiasa.

Anaeleza kuwa yupo tayari kutekeleza maridhiano ya kisiasa ambayo yapo kwa mujibu wa katiba ya Zanzibar huku akifurahishwa na kauli za baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa vya ushirikiano na serikali mpya.

"Ndugu zangu Wazanzibari uchaguzi umekwisha, nipo tayari kushirikiana na vyama vya siasa kujenga Zanzibar mpya yenye matumaini na kuweka pembeni tofauti za kisiasa.Zanzibar ni muhimu zaidi yenye kuendeleza maridhiano ya kisiasa yaliyofikiwa kwa mujibu wa katiba,"anasema na kusisitiza.

**SHEIN KIELELEZO**

Rais huyo mpya, anasema Rais aliyemaliza muda wake Dk Ali Mohamed Shein ni kigezo cha kiongozi mwenye busara na hekima ambaye daima aliweka mbele maslahi ya taifa na si vinginevyo.

"Mheshimiwa Rais mstaafu Dk.Shein nakupongeza kwa dhati kwa kuniongoza katika kipindi chote cha harakati za kampeni za uchaguzi mkuu kwa kunishauri ambapo daima utakuwa kiongozi wa mfano wa kigezo cha mafanikio yangu"anasema katika neno la shukrani.

Aidha, anawapongeza, wananchi wa Zanzibar pamoja na mabalozi wa nyumba 10 kutoka Unguja na Pemba kwa kufanya kazi kubwa ambayo imemwezesha kupata ushindi katika uchaguzi mkuu kupitia CCM.

Anawaelezea mabalozi wa nyumba 10 kuwa walisimama kidete kwa kufuatia mambo mengi ya msingi ikiwamo kuwahimiza wanachama na wafuasi wa CCM kujitokeza kwa wingi kupiga kura.

"Nachukuwa nafasi ya kipekee kuwapongeza kwa dhati mabalozi kwa kushiriki katika mchakato wa uchaguzi mkuu ikiwamo kufuatilia kwa karibu na kuona wanachama wanajitokeza kwa wingi kupiga kura."

**KUUNGANISHA WAZANZIBARI**

Vingozi wa dini wanaiomba dua kuiombea Zanzibar kuwa salama na utulivu pamoja na kumuombea Rais mpya wa Zanzibar Dk.Hussein Ali Mwinyi, kuwaunganisha Wazanzibari.

Naibu Kadhi Mkuu wa Zanzibar Sheikh Hassan Othman Ngwali, anamwombea rais huyo kuendeleza undugu wa wananchi wa pande mbili za Unguja na Pemba na kuwaunganisha na kufanya mambo yote mema yaliyofanywa na marais waliotangulia.

"Tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu upate nguvu za kuwaunganisha wananchi wote na kuendeleza umoja na mshikamano uliopo wa pande mbili za wananchi wa Zanzibar,"anasema Ngwali.

Askofu wa Anglikana Dayosisi ya Zanzibar Dk.Michael Hafidh, anamuombea Rais uongozi wenye busara na hekima wenye matarajio mengi kwa wananchi wa Zanzibar kama ahadi zake wakati alipokuwa akiomba kura katika kipindi cha mikutano ya kampeni za kisiasa.

"Tunakuombea kila la kheri katika utendaji wako ukiwa Rais wa Zanzibar, tunajua umebeba matumaini mengi ya wananchi kama alama na ahadi zako ulizokuwa ukitamka katika kipindi cha kampeni za kisiasa,'"anaomba Hafidh.



## HABARI DODOMA

# Wabunge wapya wapewa tahadhari

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WABUNGE wa Bunge lijalo, wametakiwa kuhakikisha wanawajibika ipasavyo kuisimamia serikali ili wananchi wasiwasulubu kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Akizungumza na Nipashe jana, mchambuzi wa masuala ya kisiasa na Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Dk. Leonce Mjwahuzi, alisema bunge hilo lina idadi kubwa ya wabunge wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), hivyo watambue wana deni kubwa kushinda wakati wowote.

Dk. Mjwahuzi alisema wananchi wamewapa ridhaa hiyo kwa kuwapa mafiga matatu (Rais, Mbunge na Diwani), hivyo itakuwa deni kubwa kwa chama tawala kushinda wakati mwingine wowote kwa kuwa wakiharibu hawatakuwa na mtu wa kulaumu.

"Kama kuna mtu anaingia bungeni kwa kudhani kwamba anaenda kubweteka, atambue anakwenda kwenye bunge lenye uwajibikaji kushinda wakati mwingine wowote kwa sababu wananchi wanawaangalia wanawapima kwa miaka mitano.

"Labda mambo mliyoahidi kusema mtayafanya hamjafanya kwa hiyo kura za mwaka 2025 inaweza CCM ikapata anguko ambalo halijawahi kutokea wakati wowote kwa sababu hawatakuwa na cha kujitetea," alisema.

Alibainisha watu wengi walioingia bungeni hasa wanaoingia kwa mara ya kwanza wameingia kwa mgongo wa serikali iliyomaliza muda wake kwa kuwa wao bado hawajafanya chochote.

"Kama walikuwa wanafanya chochote wameingia kwa mgongo wa mambo mengi yaliyofanywa, serikali iliyopita na wengine wamepigiwa kampeni kabisa na Rais John magufuli ambaye anaingia kwa awamu ya pili na kwa bahati mbaya au nzuri, wameingia watu wa upande mmoja wengi," alisema.

Dk. Mjwahuzi aliongeza kuwa: "Na pengine wananchi watawaambia kwamba kumbe mlijiweka wenyewe ili muunde bunge lenu peke yenu, ili kuchezea rasilimali zetu na kwa hiyo tunawapa adhabu ya kuwanyima kura."

Alisema bunge hilo la 12 linalotarajiwa kuzinduliwa hivi karibuni, litakuwa la uwajibikaji kwa kuwa Rais hatakubali kupoteza imani kwa Watanzania, hivyo wabunge wajipange kuwajibika zaidi ya wanavyodhani.

"Watu wajitahidi kutimiza ahadi za wananchi kwa sababu deni lao ni kubwa zaidi kuliko deni la tangu chama kimeingia madarakani, kwa hiyo wafanye kazi wakitambua wananchi wanawadai mambo mengi zaidi kwa sababu bungeni wapo peke yao.

"Lazima tujue bunge nimeingia na watu wa upande mmoja na kila mmoja ameingia na malengo na kero zake zinazotokana na jimbo lake, malengo ya kila jimbo hayafanani, mvutano na upinzani utakaotokea miongoni mwa chama kikubwa unaweza kuwa mkubwa kuliko tunavyodhani kwa sababu kila mtu anapeperusha bendera ya CCM, si kweli upeperushaji unafanana na jimbo moja na jingine," alisema.

"Tutarudi enzi za kina (Chrisant) Mzindakaya wakati ule kikiwa chama kimoja. Wakati huu si wakati ule kwa sababu chama kinaingiza watu wengi wa upande mmoja, lakini tufahamu wazi kwamba wapo wanachama wengi nje wa vyama vingine. Sasa hivi upinzani utakuwa mkubwa kwa sababu wameingia bungeni watu wa upande mmoja, lakini kuna watu wapo nje kuwaangalia," alisisitiza.

Alisema wakiharibu watu hao watawanyang'anya nafasi, hivyo wanatakiwa kuwajibika.

"CCM itakuwa inataka kuwahakikishia wananchi kwamba niliwaomba mafiga matatu sasa mafiga haya yanafanya kazi namna hii, kwa sababu haitoshi yeye kumaliza muda wake wa miaka mingine mitano, akaacha chama kimekufa, inamaana kitakuwa kimefia mikononi mwake na hakuna Rais anayependa kitendo hicho kitokee," alisema.

Alitoa rai kwa viongozi wa bunge hilo, kuhakikisha Bunge linasimamia serikali na kutimiza matakwa ya wananchi ambao wamewatuma kufanya kazi ya kusimamia serikali.

Kuhusu Bunge kurushwa mubashara, mchambuzi huyo alisema lilizuiwa kutokana na mambo yaliyokuwa yanaendelea ndani kinyume na utamaduni wa kitanzania. "Kwa mfano tulivyolelewa ni aibu mtu mzima kutoa tusi hadharani, kama bunge linafundisha watu na ndiyo kioo cha nchi likitoa matusi hadharani watu kutukanana na watoto na kizazi chetu kinaona mambo hayo na jamii za kimataifa zinaona hayo, inawezekana kusema Tanzania hulka yao ni hiyo," alisema.

Alisema bunge kuwa au kutokuwa mubashara itategemea nidhamu itakayokuwa inaendelea bungeni.



Vijana wa kabila la Wamasai, wakimsuka nywele mteja wao, ili kujipatia ujira wa siku, katika eneo la Mji Mpya, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wenye ulemavu waipa kongole NEC

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SHIRIKISHO la Vyama vya Walemavu Mkoa wa Dodoma (SHIVYAWATA), limeipongeza Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kwa kuondoa vikwazo kwa watu wenye ulemavu wakati wa uchaguzi mkuu, jambo ambalo limesaidia kutimiza haki yao ya kupiga kura.

Katibu wa SHIVYAWATA Mkoa wa Dodoma, Justus Ng'wantalima, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Alisema katika uchaguzi huo uliofanyika Oktoba 28, mwaka huu, NEC iliwapa kipaumbele na kuondoa vikwazo vingi vinavyokwamisha kushiriki kikamilifu kwenye upigaji kura.

"Kutokana na mazingira yaliyokuwapo, ilikuwa rahisi watu wenye ulemavu kujitokeza kupiga kura na kuchagua viongozi wanaowataka. Sisi SHIVYAWATA Dodoma, tuna kila sababu ya kuwapongeza tume kwa kuwa tumeridhika na upigaji kura mwaka huu tofauti na chaguzi za huko nyuma," alisema. Katibu huyo alitaja baadhi ya vikwazo vilivyotafutiwa ufumbuzi ni kuongezeka kwa vituo vya kupigia kura na vifaa vya kupigia kura ikiwamo karatasi za kupigia kura za nukta nundu.

Pamoja na hayo alisema kulikuwa na tatizo la miundombinu rafiki kwa baadhi ya vituo hali iliyowalazimu kubebwa ili kufikia kituo cha kupiga kura.

Alisema baadhi ya majengo ya shule ya zamani hayajarekebishwa miundombinu yao, hali ambayo watu wenye ulemavu walikutana na kikwazo hicho.

Ng'wantalima alitaja majengo hayo ambayo yalikuwa yamewekwa vituo vya kupigia kura ni pamoja na majengo ya shule ya msingi na sekondari na ofisi za serikali. Kadhalika, aliwataka watu wenye ulemavu kuhakikisha wanashiriki kikamilifu kufanya shughuli zinazowaingizia kipato, ili kuunga juhudi za serikali za kujiletea maendeleo.

## Sababu wajasiriamali kukwama zabainishwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) mkoani Dodoma limesema vikundi vingi vikiwamo vya kinamama havipigi hatua kutokana na kushindwa kutafuta masoko ya miradi wanayoifanya.

Akizungumza na Nipashe jana, wakati akitoa mafunzo ya namna ya usimamizi wa fedha na kukuza mitaji ya biashara kwa kikundi cha kinamama wastaafu wa Ujamaa ni Imani, Ofisa Uendelezaji Biashara wa SIDO Dodoma, Crispin Kapinga, alisema licha ya kutoa mafunzo kuna tatizo la kushindwa kutafuta masoko.

Kapinga alisema tatizo kubwa ambalo wamekuwa wakikutana nalo katika baadhi ya vikundi ambavyo wanavipa semina ni kushindwa kutafuta masoko ya biashara ambazo wanafanya.

Alisema tatizo hilo limekuwa likivikwamisha vikundi vingi kushindwa kupiga hatua na kushauri kutumia vijana kuwatafutia masoko.

"Hili ni tatizo kubwa sana katika vikundi vingi ndiyo maana SIDO tumekuwa tukivitembelea mara kwa mara vikundi kwa ajili ya kuwapa mafunzo," alisema Kapinga.

Alisema lengo lao ni kuona vikundi ambavyo vinachukua mikopo vinasonga mbele katika biashara zake badala ya kurudi nyuma.

Naye Mwenyekiti wa Ujamaa ni Imani, Eunice Kenyunko, alisema mafunzo waliyopata kutoka kwa SIDO, yamewasaidia kwa kiasi kikubwa kupata uelewa wa namna ya utafutaji masoko ya miradi ya biashara ambazo wanafanya.

Alisema ushauri waliopata kutoka shirika hilo, utazidi kuimarisha kikundi chao ambacho kinatarajia kuanza kuendesha mradi wa usindikaji asali.



# Aiomba serikali kuboresha barabara TANZAM

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MWENYEKITI wa Umoja wa Madereva Bajaji Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Idd Ramadhan, ameiomba serikali kuboresha miundombinu ya barabara zilizoko pembezoni mwa barabara kuu ya Tanzania na nchi ya Zambia (TANZAM), ili kupunguza foleni ambayo ni tatizo kwa watumiaji wa vyombo vya moto.

Ramadhan alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na Nipashe, alidai kuwa hali ya miundombinu ya barabara kwa jiji hilo hairidhishi kwa sababu baadhi hazipitiki, hivyo kusababisha msongamano kwenye barabara kuu.

Alisema jiji hilo lina jumla ya bajaji 3,000 ambazo hufanya safari zake kwenye maeneo mbalimbali, lakini kwa sababu ya miundombinu kuharibika hulazimika kufanya safari zinazofika hata daladala.

"Miundombinu ya barabara kwa sasa hairidhishi bajaji zinalazimika kutumia barabara kuu ambayo ina msongamano, tunaiomba serikali kuangalia upya suala hilo na mamlaka kupanga ruti mpya ili kusogeza huduma hiyo kwenye maeneo yaliyo pembezoni," alisema Ramadhan.

Vile vile, aliwaomba wagombea wote walioteuliwa kwenye nafasi mbalimbali kuanzia udiwani na ubunge kutekeleza ahadi walizozitoa wakati wakiomba ridhaa ya kuwatumikia wananchi ikiwa ni pamoja na ahadi ya kuboresha miundombinu ya barabara.

Mmoja wa madereva bajaj, Jackson Boniface, alisema kazi ya bajaji imekuwa na mchango mkubwa katika kuwasaidia wananchi kujikwamua kiuchumi.

Alisema kwa sasa vijana wengi wamepata ajira au kuajiriwa kupitia bajaji kwa kuwasaidia kuendesha maisha yao ya kila siku.

Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA), mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Denis Daud, alisema, serikali imeandaa utaratibu mzuri wa kuhakikisha wanatengeneza miundombinu safi kwa ajili ya bajaji.

Aliwaomba madereva hao kuzingatia kanuni na taratibu za usalama barabarani, ili kuepusha usumbufu na ajali ambazo zinaepukika.

# Mchakato Mbeya kuwa manispaa mbili waanza

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MCHAKATO wa kuigawa Halmashauri ya Jiji la Mbeya kuwa na manispaa mbili umekamilika baada ya viongozi kukamilisha taratibu zote zinazohitajika kwa mujibu wa sheria.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, aliyasema hayo jana wakati wa kikao kilichowakutanisha viongozi wa dini, watumishi na wakuu wa vyuo pamoja na wawakilishi madereva bajaji na bodaboda katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya.

Chalamila alisema mchakato huo umekamilika baada ya Rais mteule wa Tanzania, Dk. John Magufuli, wakati wa kampeni zake kuahidi jiji hilo kuligawa na kupata manispaa mbili.

Alisema Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji, Amede Ng'wanidako, pamoja na wataalamu wa mipango miji walienda kujifunza namna ya kukamilisha mchakato huo.

"Tunayo furaha kubwa kuwaambia kuwa tayari tumeanza mchakato wa kuigawa Halmashauri ya Jiji la Mbeya kuwa manispaa mbili lengo ni kuleta maendeleo kwa wananchi, ambapo kupitia manispaa hizo miundombinu ya barabara, hospitali, shule na taasisi zote muhimu zitajengwa," alisema Chalamila.

Alisema lengo la kuigawa halmashauri kupata manispaa mbili kulipa hadhi Jiji la Mbeya ambalo kwa kipindi kirefu halikuwa na maendeleo makubwa ikilinganishwa na majiji mengine ambayo yamepiga hatua kubwa.

Katika hatua nyingine, Chalamila aliwaomba viongozi wa dini kufanya maombi ya pamoja kwa kipindi cha mwezi mmoja kumwombea Rais mteule Dk. Magufuli ili kuendelea na kasi aliyoanza nayo katika awamu ya tano. Alisema maombi hayo yatasaidia kumpa nguvu Magufuli kuendelea na spidi ya awali katika kuwatumikia wananchi na kuongeza nidhamu kwa watumishi, pia kudhibiti mianya ya rushwa.

Mwakilishi wa wabunge wateule wa Mkoa wa Mbeya, Anthon Mwantona, aliwaahidi Wanambeya kuwa kazi kubwa watakayoifanya wabunge hao ni kupeleka matatizo ya wananchi bungeni ili yatatuliwe.

Alisema kwa umoja wao watakuwa kielelezo kizuri katika kusimamia na kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo yatachangia Mkoa wa Mbeya kuwa wa mfano bila kujali itikadi za kisiasa.



Mwenyekiti wa Wafanyabiashara wa Mkoa wa Mbeya, Jeremiah Mahenge, akitoa neno ya shukrani katika mkutano ulioandaliwa na Mkuu wa Mkoa huo, Albert Chalamila (hayupo pichani), jijini humo jana, kwa ajili ya kuwashukuru viongozi wa dini na kada mbalimbali kwa kuliombea taifa na kufanya uchaguzi mkuu ufanyike kwa amani na utulivu. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# DC awaomba wananchi kuyapuuza maandamano

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

MKUU wa Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, Mayeka Simon, amewaomba wananchi kuyapuuza maandamano yanayoendelea kuratibiwa na baadhi ya wanasiasa kupinga matokeo ya uchaguzi mkuu yaliyofanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Mayeka alitoa ombi hilo jana, baada ya kuwapo kwa uvumi kwamba baadhi ya vyama vya siasa vinaratibu maandamano kupinga matokeo ya uchaguzi wakidai haukuwa huru na haki.


Aliwaomba wananchi kuendelea na shughuli zao za uzalishaji mali badala ya kukaa vijiweni au kwenye maeneo mengine kuratibu maandamano.

"Nawatahadharisha wale wote wanaotaka kufanya maandamano ndani ya wilaya yao naomba msijaribu kwa sababu tumejipanga, uchaguzi umekwisha sasa ni wakati wa wananchi kuchapa kazi," alisema Mayeka.

Alisema Wilaya ya Chunya inashughuli nyingi za kiuchumi zikiwamo za kilimo, ufugaji, uchimbaji wa madini na biashara hivyo kufanya maandamano yasiyo na tija ni kuzorotesha uchumi. Alisema moja ya fursa kubwa ambayo inaipaisha Wilaya hiyo kuongeza pato kubwa ni madini ya dhahabu na kwa umuhimu huo serikali ilifungua soko la madini, ili wafanyabiashara na wachimbaji waweze kuuza na kununua katika soko la pamoja.

Kadhalika, alisema hadi sasa soko hilo linaendelea kufanya vizuri baada ya kufanyika kwa marekebisho ya sheria ya madini ambayo pia inaruhusu kufunguliwa kwa masoko madogo kwenye vituo vya shughuli za uchimbaji. Mwenyekiti wa wachimbaji Mkoa wa Mbeya (MBEREMA), Leonard Manyesha, alisema kamwe wachimbaji hawaungi mkono maandamano yoyote yanayoratibiwa na baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa na kwamba wameridhika na viongozi walioteuliwa kwa sababu walichaguliwa kwa mujibu wa katiba na sheria.

Katibu wa MBEREMA, Robert Msowoya, alisema hivi sasa uchaguzi umeisha na nguvu zao wanaelekeza kwenye shughuli za uzalishaji na kuhimiza kudumisha amani.



# CCM wajificha kuteua mgombea wa uspika Baraza la Wawakilishi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU Mwenyekiti wa CCM na Rais mstaafu wa Zanzibar, juzi aliongoza kikao maalum cha Kamati Maalum ya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) Zanzibar.

Kikao hicho kilifanyika Ofisi Kuu ya Chama Kisiwandui, ambapo pamoja na mambo mengine, kilijadili mapendekezo ya wana CCM wanaoomba kuteuliwa kugombea nafasi ya Spika wa Baraza la Wawakilishi.

Kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, Ibara ya 73, Spika wa Baraza la Wawakilishi anaweza kuchaguliwa kutoka miongoni mwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi au mtu mwenye sifa za kuchaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Pia kwa mujibu wa Kanuni ya Tano ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, toleo la mwaka 2020, kila chama cha siasa chenye usajili wa kudumu kinaweza kushiriki katika uchaguzi wa spika kwa kuwasilisha jina la mgombea wake.

CCM inawajibika kufanya mchakato wa ndani ili kupata jina la mwanachama atakayegombea nafasi hiyo katika Baraza la Wawakilishi linalotarajiwa kuzinduliwa hivi karibuni.

Kikao hicho kilipokea na kujadili majina ya wanachama waliojitokeza kuomba kuteuliwa kugombea nafasi ya uspika.

Pia kikao hicho kitatoa mapendekezo yake kuhusu wanachama wanaoomba kuteuliwa kugombea nafasi ya uspika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwa Kamati Kuu ya NEC ambayo itateua jina la mwanachama mmoja atakayegombea nafasi hiyo. Akizungumza wakati wa kikao hicho, Dk. Shein alisema matokeo ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu yamevunja rekodi toka enzi za Chama cha ASP hadi sasa wakati wa mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Dk. Shein alisema wagombea wote wa CCM walikuwa imara na wana sera zinazouzika kwa wananchi.

Hata hivyo, hayo aliwasihi wajumbe hao kutobweteka na ushindi uliopatikana badala yake waanze mapema kujiandaa na uchaguzi ujao baada ya miaka mitano.

Aliwashukuru wana CCM wote na wananchi kwa ujumla waliofanya uamuzi sahihi wa kuichagua CCM, ili iwaletee maendeleo endelevu kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Kiongozi huyo alisema amefika ukomo wa utumishi wake wa urais kwa mujibu wa matakwa ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na kumkabidhi mrithi wake, Dk. Hussein Ali Mwinyi, nchi ikiwa katika mikono salama ya CCM. Aliwataka kuendelea kulinda tunu za Muungano na Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Abdulla Juma Mabodi, alisema CCM ina deni kwa wananchi la kutekeleza ahadi zake pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-25.

Kikao hicho pia kimehudhuriwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi.



Mwenyekiti wa Chama cha Wahasibu Tanzania (TAA), Peter Mwambuja (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mkutano mkuu wa chama hicho, utakaofanyika Novemba 12 hadi 13, 2020, jijini humo. Katikati ni Mwenyekiti wa Maandalizi ya mkutano huo, Odemari Rushita na Ofisa Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma, Winnie Ngaraguza. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Wananchi Pemba kupata umeme

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SHIRIKA la Umeme Zanzibar (ZECO) limewataka wananchi kijiji cha Makoongwe Mkoa wa Kusini Pemba ambao hawajapatiwa huduma ya umeme kuanza maandalizi ya kupokea huduma hiyo.

Ofisa Mipango na Utafiti wa Shirika hilo, Ali Faki Ali, alisema hayo wakati akizungumza na wananchi wa Makoongwe kutokana na kukubali ombi la kupatiwa umeme kwa njia ya mkopo.

Alisema vijiji vyote vilivyomo ndani ya kisiwa hicho, vilipatiwa huduma hiyo lakini sasa tayari kumeshakuwa na vijiji vipya vinavyohitaji kupatiwa umeme.

Ali alisema watu 126 wako tayari kwa hatua ya kwanza kupatiwa umeme huo, ambapo watapatiwa kwa njia ya punguzo.

Pia aliwataka wananchi kufahamu kuwa lengo la shirika ni kutoa huduma kwa wananchi wote kuhakikisha wananufaika na huduma ya umeme, hivyo wananchi wanapaswa kuilinda na kuitunza miundombinu.

Naye Ofisa Uhusiano na Huduma kwa Wateja, Amour Salum, alisema ushirikiano uliopo baina ya wananchi na shirika hilo ndio utakaosaidia shirika kupiga hatua za kimaendeleo.

Aliwatata wananchi kuilinda miundombinu ya umeme ili kuwa endelevu na kunufaika na huduma ya umeme wa uhakika.

Salum alisema kuna baadhi ya wananchi wanachimba mchanga karibu na nguzo za umeme pamoja na wanaochukua mchanga katika fukwe za bahari, ambapo kebo ya umeme mkubwa imepita maeneo hayo.

Alisema pia kuna tatizo la ukataji wa miti katika laini kubwa za umeme jambo ambalo linaweza kuhatarisha maisha ya wananchi na kusababisha majanga hapo baadaye.

# Umoja wa wapinzani wasema sasa ni kazi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

UMOJA wa baadhi ya vyama vya upinzani vilivyoshiriki uchaguzi mkuu umesema uchaguzi umekwisha, hivyo wananchi wasipoteze muda kujadili na badala yake kufanya harakati zao za kimaisha.

Akizungumza na waandishi wa habari kwa niaba ya wagombea wenzake jana, aliyekuwa mgombea urais wa Zanzibar kupitia Chama cha Demokrasia Makini, Ameri Hassan Ameir, alisema uchaguzi mkuu ulikuwa wa huru na haki.

Kutokana na hali hiyo, alisema wanakubaliana na matokeo ya uchaguzi huo yaliyotolewa na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC). Alisema wako tayari kushirikiana na Rais mpya wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, katika kuiletea Zanzibar maendeleo.

"Uchaguzi umeisha sisi baadhi ya vyama vya siasa tulioshiriki uchaguzi tunaahidi kuwa tutashirikiana na Rais ili kudumisha amani ya nchi," alisema Ameir ambaye ni mwenyekiti wa chama hicho.

Alisema wananchi wa Zanzibar wametumia haki yao ya kikatiba na ya kidemokrasia kupiga kura na kumchagua kiongozi anayefaa. Katika uchaguzi huo, Dk. Mwinyi aliibuka na ushindi.

Kwa mujibu wa Ameir, kuna maisha baada ya uchaguzi, hivyo ni vyema kumsaidia Rais ili kutekeleza ahadi alizozitoa kwa wananchi wakati wa kampeni.

Pia aliwataka wawakilishi na wabunge wateule walioshinda katika uchaguzi huo, baada ya kuapishwa kuhakikisha wanarudi majimboni kwa lengo la kutekeleza ahadi walizozitoa na kutatua kero zinazowakabili wananchi.

Aliwataka viongozi hao kutekeleza majukumu yao ipasavyo na kuacha kufanya kazi kwa mazoea, ili kumsaidia Rais katika utekelezaji wa majukumu yake ya kuleta maendeleo kwa wananchi.

Sambamba na hayo, aliwataka wale wote watakaobahatika kuteuliwa na Rais kwa nafasi mbalimbali serikalini kuwa wazalendo na kutoweka maslahi yao mbele na badala yake kuwatumikia wananchi.

Naye aliyekuwa mgombea urais wa Zanzibar kupitia Tanzania Labour Party (TLP), Hassan Juma Salum, alisema uchaguzi umekwisha, hivyo ni vyema kushikamana pamoja kuijenga Zanzibar na kusonga mbele. Alisema Rais aliyeshinda ni rais wa wananchi wote na wala si rais wa CCM, hivyo ni vyema kumpa ushirikiano katika utekelezaji wa kazi zake.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

Nipashe

NIPASHE NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE NASI
KWA BEI NAFUU SANA

Nipashe

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA CHETI



115974601

**EMANUEL G. BARBAYDU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye Index No. **S1230/0121.**Kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa mwaka 2016 MAGHANG SECONDARY. Cheti cha kuzaliwa cha 12/06/1997, cheti cha JKT MAKUTUPORA DODOMA kilichotolewa mwaka 2019.
Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo karibu naye . Polisi taarifa: **ARU/ARU/RB/443794/2019.**

## KUPOTELEWA NA CHETI



115974502

**AWAMBA NGUNGA TEPANI** Amepotelewan na cheti cha kidato can ne chenye index namba **P.1577/0004/2017** kilichotolewa na shule ya secondary FANAKA MEMORIAL mwaka 2017 yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **WMB/RB/1055/2020**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FLORIAN MSIGWA**
ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA **TOYOTA BREVIS** YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 214 DCX.** Chassis namba **JCG100043726.** Engine namba **IJZ4965001.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.
TAARIFA YA POLISI: **DAR/059/RB/615568/2020.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA WILAYA YA KINONDONI**

**SHAURI LA MIRATHI NA 77 YA 2020**

**Maombi ya barua ya usimamizi wa mirathi ya marehemu MARY NGIWESAU NA MWOMBAJI LILIAN THEODORE LYIMO**

**TAARIFA YA KAWAIDA.**
**KANUNI 75**

Watu wote wanaodai kuwa na haki na mali za marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hilikatikaq jaladab kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa baruab ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mbnamo aun kabla ya tarehe 27/10/2020

**Hati hii imetolewa 09/10/2020**

115974102

## KUPOTEA KWA VYETI



115974302

**ZAINABU YAHAYA BAKARI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.3715/0211** kilichotolewa na BUZA SEKONDARI mwaka 2015. Cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P3549/0006** kilichotolewa na **BRAIN TRUST SEKONDARI CENTRE** mwaka 2016. Cheti cha kidato cha nne chenye index namba P3549/0044 kilichotolewa na BRAIN TRUST SEKONDARI CENTRE mwaka 2017. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CHA/RB/641658/2020.**

## KUPOTELEWA NA VYETI



115973302

**INNOCENT MODEST TIBAIKANA**, Amepotelewa na vyeti cha kidato cha nne chenye index namba **S0461-0051** kilichotolewa mwaka 2002 na shule ya secondary KAHAMA na cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0773-0660 kilichotolewa na shule ya **MWENGE OPEN ACADEMY** yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi, Polisi taarifa **OB/RB/8976/2015**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**LUCY ELIAS MUSHI**
anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Toyota yenye namba za usajili **T.339 CZL.**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.Taarifa ya polisi **MBE/MBE/RB/773325/2020**

115974202

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**MWESIGWA'S AGROVET CO. LTD**

**REGISTRATION NO. 52356**

**RESOLUTION TO WIND UP THE COMPANY**

**DATED 02nd DAY OF November 2020**

**THE SHAREHOLDERS/MEMBERS** of the above named company passed the following special resolution:

i. **WINDING UP OF THE COMPANY**
   **IT WAS SO RESOLVED** by this special resolution, the company be wound up voluntarily.
ii. **APPOINTMENT OF A LIQUIDATOR**

**THAT,** Advocate **GIRARYOBA MAKAZA** of Elly Attorneys, of P.O. Box 10064 Mwanza be and is hereby appointed as Liquidator for purposes of such winding up.

The above is a certified True Copy of the Resolution of the Shareholders Meeting

**Dated this 02nd Day of November, 2020.**

Uza,
Chenye
Thamani
Kubwa Kwa
Kutangaza
Nasi
Kwa Bei Poa
Tupigie
0782253676

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Wamarekani kuamua kati ya Trump na Biden

**WASHINGTON, Marekani**

WAMAREKANI wamepiga kura jana kumchagua Rais mpya kati ya Donald Trump wa Republican anayewania muhula wa pili au mpinzani wake wa chama cha Democratic, Joe Biden.

Kutokana na kampeni zilizokuwa na ushindani mkali, raia wa Marekani walipiga kura jana kumchagua Rais mpya kati ya hao.

Uchaguzi huo umefanyika katika wakati ambapo janga la virusi vya corona limesababisha vifo vya takriban watu 230,000, na mamilioni wengine kupoteza ajira.

Ingawa siku hiyo ndiyo rasmi ya uchaguzi, watu wapatao milioni 100 tayari wameshapiga kura ya mapema.

Hadi hii jana, Biden anaonekana kuwa mbele ya Trump katika majimbo kadhaa, kulingana na maoni ya wapiga kura.

Hata hivyo, mbali na kura za raia, mgombea urais atahitajika kupata angalau kura 270 za wajumbe maalum ili kushinda kinyang'anyiro cha urais nchini Marekani.

*DW*




Donald Trump anatafuta muhula wa pili urais Marekani. **PICHA: MTANDAO**

# Bobi Wine ateuliwa na Tume kugombea

**KAMPALA, Uganda**

MGOMBEA Urais, Robert Kyagulanyi, maarufu kama Bobi Wine, alibebwa na polisi baada ya kuthibitishwa kuwa mgombea na Tume ya Uchaguzi, kwa mujibu wa mwandishi wa habari wa BBC, Patience Atuhaire.

"Bobi Wine alichukuliwa na polisi mara baada ya kumalizika kwa shughuli ya uteuzi wake na kupelekwa moja kwa moja hadi nyumbani kwake," Atuhaire alisema.

Wafuasi wa mwanasiasa huyo walikuwa wamekusanyika nje ya kituo cha uteuzi huku wengine wakiwa wanamsubiri barabarani. Awali, polisi walikuwa wametangaza masharti makali kuhusu idadi ya wafuasi wanaoruhusiwa kuandamana na mgombea urais hadi tume ya uchaguzi kuwasilisha stakabadhi zake.

Wafuasi wake waliokuwa wamekusanyika katika makao makuu ya chama chake cha National Unity Platform kwa ajili ya kuzinduliwa kwa manifesti yao walitawanywa kwa vitoza machozi.

Bobi Wine anakabiliana na wagombea wengine tisa kwenye kinyang'anyiro hicho akiwamo Rais Yoweri Museveni katika uchaguzi wa mwaka ujao.

*BBC*

## Upinzani kuunda serikali ya mpito

**ABIDJAN, Coast**

UPINZANI nchini Ivory Coast umesema kuwa unaunda serikali ya mpito baada ya kususia uchaguzi wa urais Jumamosi kwa sababu ya uamuzi wa Rais Alassane Ouattara wa kuwania muhula wa tatu.

Kiongozi wa upinzani, Pascal Affi N'Guessan alisema moja ya majukumu ya serikali ya mpito itakuwa kuandaa uchaguzi wa haki, uwazi na wenye kujumuisha kila mmoja.

N'Guessan alisema baraza la taifa la mpito limeundwa ambalo litamteua aliyekuwa rais wa nchi hiyo, Henri Konan Bédié, kuongoza serikali ya mpito ambaye pia ni kiongoni wa chama cha Democratic nchini humo.

"Kumuendeleza Ouattara kama kiongozi wa taifa kuna uwezekano mkubwa wa kusababisha vita vya ndani wa ndani,"N'Guessan alisema.

Chama tawala kimeonya upinzani dhidi ya jaribio lolote la kusababisha vurugu nchini humo.

Takribani watu 9 wameuawa wakati wa uchaguzi, huku waandamanaji wa upinzani wakijaribu kuzuia watu kupiga kura.

**BBC**

# Watu 32 wauawa kwa kupigwa risasi

**ADDIS ABABA, Ethiopia**

WATU waliokuwa na silaha wameua wananchi karibu 32 na kuchoma moto nyumba katika shambulio baya huko magharibi mwa Ethiopia, maofisa wamesema.

Mamlaka ya eneo ilisema kuwa waasi wa Jeshi la Oromo Liberation Army linafaa kulaumiwa kwa shambulizi hilo lililotokea jimbo la Oromia.

Wakazi walisema kuwa makumi ya watu walikusanywa na kuuliwa huku mifugo yao ikiibwa.

Waziri Mkuu, Abiy Ahmed alisema huenda shambulizi hilo limehusika na suala la ukabila.

Ghasia za kikabila zimekuwa zikiongezeka tangu alipoingia madarakani Aprili 2018.

Ofisa wa eneo aliiambia BBC kwamba kuna timu iliyotumwa Guliso eneo la tukio kufanya uchunguzi huku ikikisiwa kwamba idadi ya waliokufa huenda ikaongezeka.

Tume ya Haki za Binadamu Ethiopia ilisema watu wa kabila la Amharic, kundi ambalo ni la pili kwa ukubwa limelengwa kwenye shambulio hilo lililofanyika Jumapili.

Aidha, mwenyekiti wa tume ya Umoja wa Afrika, Moussa Faki Mahamat, ameshtumu mauaji hayo.

Katika taarifa yake, Faki Mahamat, amewasihi kujizuia kufanya fujo na kutoa wito wa majadiliano.

**BBC**




# PIRES
## AMPELEKA MBAPPE MADRID

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe anatakiwa kujiunga na Real Madrid kama anataka kuendelea kukua kama mchezaji, kwa mujibu wa nyota wa zamani wa Ufaransa, Robert Pires.

Mbappe mwenye umri wa miaka 21, amekuwa akihusishwa sana na kuhamia Madrid baada ya kung'ara pale Paris Saint-Germain, ambako ana mkataba hadi mwaka 2022.

Pires, ambaye alikataa kuichezea Madrid kipindi chake cha uchezaji, amesema Mbappe anatakiwa kujiunga na miamba hao wa LaLiga - na nyota huyo wa zamani wa Arsenal na Ufaransa analiona hilo linawezekana kabisa.

"Bila shaka. Mimi ni Mfaransa, naipenda Paris Saint-Germain na napenda yeye kubakia kwenye Ligue 1," alisema akiiambia AS.

"Lakini endapo anataka kuendelea kukua kama mchezaji, anatakiwa kusajiliwa Real Madrid."

Kocha wa Madrid, Zinedine Zidane awali alibainisha namna gani anavutiwa na Mbappe, ambaye ana mabao sita na pasi za mwisho tano katika mechi saba msimu huu.

Mbappe alitoa pasi za mwisho mbili kwa Moise Kean wakati PSG wakiibuka na ushindi wa mabao 2-0 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Istanbul Basaksehir, Jumatano.

Tangu kuanza kwa msimu wa 2017-18, Mbappe ana pasi za mwisho nyingi zaidi (15) kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kuliko mchezaji mwingine yeyote.

Zidane pia amekuwa kwenye presha pale Madrid baada ya kushinda mechi moja kati ya nne zilizopita katika mashindano yote. "Nafikiri ni watu wasiofikiria wanazungumza kuhusu zama za mwisho za Real Madrid wakati inapopoteza mechi mbili kabla ya Clasico na sare dhidi ya Borussia Monchengladbach," alisema Pires.

"Najua kuna presha kubwa Madrid, lakini kocha na wachezaji wanahitaji kutulizwa kwa sababu kufungwa ni sehemu ya mchezo.

## MARADONA HALI TETE

**BUENO AIRES, Argentina**

GWIJI wa soka wa Argentina, Diego Maradona, ameripotiwa kukimbizwa hospitali kutokana na kutokuwa fiti kwa afya yake, huku kukiwa hakuna maelezo zaidi kuhusu kinachomsumbua.

Maradona, mwenye umri wa miaka 60, alipelekwa hospitali kufanyiwa vipimo baada ya kujihisi vibaya kutokana na afya yake kutokuwa kwenye ubora.

Gwiji huyo anakumbukwa kwa uwezo wake ndani ya uwanja pamoja na vituko vyake, ambapo akiwa na timu ya Taifa ya Argentina alikiongoza kikosi hicho kutwaa taji la Kombe la Dunia mwaka 1986 na anatajwa kuwa mchezaji bora wa muda wote ndani ya Taifa la Argentina.

Daktari wa Maradona, Leopoldo Luque, amesema nyota huyo wa zamani wa Argentina, alijisikia vibaya ghafla jambo lililofanya afanyiwe vipimo ili kujua kinachomsumbua.

"Amekuwa akijihisi vibaya ila ninaamini kwamba baada ya kufanyiwa vipimo kila kitu kitawekwa wazi na tatizo lake litajulikana, hayupo sawa kiafya, hayupo sawa labda baada ya muda tutajua mambo yatakuaje," alisema akinukuliwa na BBC Sport.

## KOULIBALY HATAKI KUONDOKA NAPOLI

**NAPLES, Italia**

KALIDOU Koulibaly amesisitiza anaipenda Napoli, lakini amesema "tutaona nini kitatokea" wakati huu kukiwa na uvumi kuhusu majaliwa yake klabuni hapo.

Koulibaly mwenye umri wa miaka 29, mara kwa mara amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka kwa miamba hao wa Serie A, huku Liverpool ikiripotiwa kumwania mlinzi huyo.

Beki huyo wa kati wa kimataifa wa Senegal, ambaye mkataba wake na Napoli unamalizika mwaka 2023, anatambua namna anavyohitajika, lakini amesema anaipenda klabu hiyo ya Italia.

"Naipenda Naples na watu wa Naples wananipenda mimi, hilo ndio jambo muhimu zaidi," alisema Koulibaly kupitia Sky Sport, baada ya timu yake kushinda bao 1-0 dhidi ya Real Sociedad kwenye Ligi ya Europa.

"Mara zote nakuwa tayari katika kila mchezo, bado nina mkataba wa miaka mitatu, nimetulia, timu zinaniwania mimi, lakini bado nipo hapa.

"Nacheza katika kiwango changu cha juu na kuisaidia timu na watu hawa kwa sababu nataka kuwapa kitu fulani wao, halafu tutaona nini kitatokea."



## HABARI MICHEZO




# HAALANDA
## ATATUA LIVERPOOL - FREUND

**LIVERPOOL, England**

NYOTA wa Borussia Dortmund, Erling Haaland, atatua kwa mabingwa wa Ligi Kuu ya England, Liverpool, kwa mujibu wa Mkurugenzi wa Michezo wa Salzburg, Christoph Freund.

Haaland haraka amejiimarisha yeye mwenyewe kama mmoja wa washambuliaji bora zaidi duniani, akiwa amechomoza kutoka kwa mabingwa wa Austria, Salzburg kabla ya kujiunga na miamba wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, Dortmund, Januari mwaka huu.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 20, amefunga mabao 44 katika mashindano yote msimu wa 2019-20 - 16 kati yake yakipatikana katika mechi 18 alizocheza Salzburg kabla ya kutua Dortmund.

Haaland tayari ana mabao matano kwenye Bundesliga msimu huu, huku akiwa amefunga mabao nane katika mashindano yote.

Freund anaamini raia huyo wa Norway atajiunga na Liverpool wakati akihusishwa pia na Manchester United, Real Madrid na Juventus.

"Huko ndio anatakokwenda," amesema Freund akiiambia Sky Sports baada ya gwiji wa Bayern na Ujerumani, Lothar Matthaus kusema kwamba, Liverpool ndio sehemu inayomfaa.

"Anaweza kucheza katika klabu yoyote duniani. Hasa kutokana na uwezo wake na kujiamini na ana miaka mingi zaidi ya kutamba kwenye soka."

## NUNEZ AWANIWA BARCA KUVAA VIATU VYA SUAREZ

**BARCELONA, Hispania**

KLABU ya Barcelona inafikiria kumsajili nyota wa Benfica, Darwin Nunez, kama mrithi sahihi wa Luis Suarez, kwa mujibu wa ESPN.

Nunez alijiunga na Benfica Septemba, mwaka huu, lakini tayari majaliwa yake ndani ya klabu hiyo yanaonekana kutokuwa makubwa.

Nunez amekuwa na kiwango cha kuvutia sana kule Benfica, ambapo kocha Jorge Jesus amemtaja nyota huyo mwenye umri wa miaka 21, kama ndiye mrithi sahihi wa Joao Felix aliyesajiliwa na Atletico Madrid mwaka jana.

Kwa mujibu wa ripoti, Barcelona wanaona kwamba nyota huyo wa kimataifa wa Uruguay ndiye anaweza kuziba pengo la Suarez.

Nunez alikuwa mchezaji aliyesajiliwa kwa fedha nyingi zaidi pale Benfica akitua kwa pauni milioni 24 kutoka Almeria na tayari amefunga mabao manne tangu atue nchini Ureno.

Barca awali ilitaka kumsajili Nunez kutoka Almeria na sasa imejiweka kwenye nafasi nzuri zaidi ya kumsajili.

## FERDINAND AMJIA JUU MAGUIRE UTD

**MANCHESTER, England**

NYOTA wa zamani wa Manchester United, Rio Ferdinand, amehoji uwezo wa nahodha Harry Maguire wakati akitoa maoni yake baada ya timu hiyo kupoteza mchezo dhidi ya Arsenal kwenye Ligi Kuu England.

Maguire akiwa ndani ya kikosi cha United alikumbana na kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Arsenal Jumapili ikitoka kushinda mabao 5-0 dhidi ya RB Leipzig wiki iliyopita kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

United ambao wapo nafasi ya 15 kwenye msimamo wa Ligi Kuu, wamekusanya pointi saba tu katika mechi sita za msimu huu.

Ferdinand, mshindi mara sita wa Ligi Kuu na mara moja Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na United amemtaka, Maguire kuonyesha uongozi wake pale Old Trafford.

"Tunakosa kujiamini katika maeneo fulani. Timu inaonekana kama vile haina kiongozi," alisema Ferdinand akinukuliwa na BBC Sport.

"Nimemwona Harry Maguire katika mechi nyingi na inaonyesha kama ni mtu asiyejiamini na ambaye hajui kabisa kazi yake kama kiongozi, anatakiwa kuibeba timu kama nahodha."

Kikosi hicho cha kocha, Ole Gunnar Solskjaer leo, Jumatano kitacheza na Istanbul Basaksehir kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA AIKATAA MAZIMA BARCELONA

Muda wangu pale umekwisha, kocha aliyepo kwa sasa, Ronald Koeman ninamheshimu, ni rafiki...

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola amesisitiza kuwa muda wake katika klabu ya Barcelona umekwisha baada ya kocha huyo wa Manchester City kuhusishwa na uhamisho wa kurudi kwa miamba hao wa Hispania.

Mgombea wa urais katika klabu ya Barcelona, Victor Font, amesema anafikiria kumrudisha Guardiola iwapo atachaguliwa.

Guardiola aliisaidia klabu hiyo kushinda mataji 14 wakati akiwa kocha pale.

"Kabla ya kuondoka mwaka 2012, kama kocha, muda wangu kuifundisha Barcelona umekwisha," alisema Guardiola akinukuliwa na gazeti la Daily Mail.

"Nilihudumu muda wangu katika klabu hiyo. Kocha aliyepo kwa sasa, Ronald Koeman yupo na ninamheshimu. Ni rafiki yangu mzuri sana."

Guardiola alikuwa akizungumza baada ya timu yake ya Man City kuilaza klabu ya Sheffield United bao 1-0 katika mchezo wa Ligi Kuu England.

Ilikuwa mechi ya tatu ya City katika wiki moja baada ya sare na West Ham kufuatiwa na ushindi wa 3-0 dhidi ya Marseille katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Tulicheza vema sana," aliongeza Guardiola. "Tulipata wakati mgumu kuweza kupata goli ikilinganishwa na nafasi tulizotengeneza, mashambulizi 16, nane yakilenga goli, ni mchezo mzuri dhidi ya timu.

"Ni mechi ya tatu katika siku saba, zote zikiwa ugenini. Jambo la muhimu ni kwamba tulipata ushindi."

## KWA UFUPI

### CITY WAKOMAA NA MESSI

KLABU ya Manchester City inaweza kumpa ofa ya mkataba wa awali mshambuliaji wa Barcelona na Argentina, Lionel Messi mwenye umri wa miaka 33, kabla ya kuhamia England msimu ujao. ***(Daily Telegraph)***

### CONTE AIANIKA REAL MADRID

KOCHA wa Inter Milan, Antonio Conte, mwenye miaka 51, amesema alikacha mara mbili nafasi ya kuifundisha Real Madrid kwa kuwa hakutaka kuchukua jukumu hilo kwa timu ambayo tayari ilishauanza msimu wake. (Marca)

### RAHEEM, DE BRUYNE KUONGOZA

MANCHESTER City wanajiandaa kumfanya mshambuliaji wa England, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 25 na kiungo wa kati wa Ubelgiji, Kevin de Bruyne mwenye miaka 29 kuwa wachezaji wanaolipwa fedha nyingi zaidi katika Ligi ya England. ***(90 Min)***

### LAMPTEY AGOMBEWA

KLABU ya Atletico Madrid ipo kwenye mbio moja na Bayern Munich na Sevilla kumwania beki wa kulia wa Brighton, Tariq Lamptey mwenye miaka 20. ***(Mail)***

### CHUKWUEZE AWINDWA EPL

MANCHESTER United, Leicester na Everton wanamwania winga wa Nigeria anayekipiga Villarreal, Samuel Chukwueze, mwenye miaka 21. ***(90 Min)***

### PSG BADO KWA DELE ALLI

KLABU ya Paris St-Germain itakuwa makini katika uhamisho wa mchezaji wa England anayekipiga Tottenham, Dele Alli, mwenye umri wa miaka 24, ikiwa atapatikana Januari mwakani. Klabu hiyo ya Ufaransa ilifanya majaribio matatu yaliyogonga mwamba ya kumsajili kwa mkopo kiungo huyo wa kati msimu huu. ***(Mail)***

### NUNEZ AWANIWA BARCELONA

BARCELONA imeongeza nia yake ya kutaka kumnasa mshambuliaji wa Benfica na Uruguay, Darwin Nunez mwenye umri wa miaka 21, kama mbadala wa muda mrefu wa Luis Suarez. ***(ESPN)***

### BARCA YAMFUKUZIA GARCIA

BARCELONA itatoa ofa mpya ya pauni milioni saba kwa mchezaji wa nafasi ya ulinzi Hispania, Eric Garcia, Januari mwakani. ***(ESPN)***

### USAJILI WA DEPAY HATIHATI

KUJIUZULU kwa Josep Maria Bartomeus katika nafasi ya urais pale Barcelona kunaweza kufanya mpango wa uhamisho wa Garcia au mshambuliaji wa Lyon, Mamphis Depay, mwenye miaka 26 kuwa mgumu Januari. ***(Marca)***

### ALABA AIKOSOA BAYERN

MLINZI David Alaba mwenye umri wa miaka 28, ameikosoa Bayern Munich baada ya kugundua kuwa klabu imeondoa ofa yao ya mkataba mpya. Mkataba wa mchezaji huyo wa nafasi ya ulinzi utakwisha mwishoni mwa msimu huu. ***(Mail)***

### PSG YAMTAJA ALCANTRA

KLABU ya Paris St-Germain ilitaka kumsajili, Thiago Alcantara mwenye umri wa miaka 29, msimu huu, lakini badala yake iliishia kwa kaka yake Rafinha mwenye miaka 27, baada ya kiungo huyo wa kati kuondoka Bayern Munich na kwenda Liverpool. ***(France Football)***

### ANCELOTTI KUMVUTA ISCO

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Isco, mwenye umri wa miaka 28, anahusishwa na kwenda kujiunga na bosi wake wa zamani, Carlo Ancelotti, na mchezaji mwenzake wa zamani, James Rodriguez pale Everton. ***(Sunday Mirror)***

### GATTUSO KUULA TENA NAPOLI

KOCHA Gennaro Gattuso anakaribia kusaini mkataba mpya na Napoli, wakati huu ule wa sasa ukitarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Sky Italia)***

## HABARI MICHEZO

# POLISI TANZANIA WAZITAKA TATU ZA MBEYA CITY KESHO

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kuvuna pointi tatu katika Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga dhidi ya Tanzania Prisons, kikosi cha Polisi Tanzania jana, kimewasili salama jijini Mbeya tayari kusaka alama zingine tatu kutoka kwa Mbeya City kesho, Alhamisi.

Polisi Tanzania ambayo Jumamosi iliibuka na ushindi wa bao 1-0 ugenini dhidi ya Prisons ulioiwezesha kufikisha pointi 14 na kukaa katika nafasi ya saba kwenye msimamo wa Ligi Kuu, kesho itashuka katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya kuwavaa wenyeji wao, Mbeya City ambao juzi walilazimishwa sare ya bao 1-1 na majirani zao, Ihefu FC.

Akizungumza na mwandishi wetu kwa simu kutoka Mbeya, Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini, alisema wamejipanga kupata pointi tatu kwenye mchezo huo, ambao anaamini utakuwa na ushindani mkubwa.

Alisema mara nyingi wanapokutana na Mbeya City huwa haikubali kupoteza ikiwa nyumbani, lakini anaamini wanaweza kupata matokeo mazuri.

"Tunaendelea na mazoezi kuhakikisha tunapata ushindi tukiwa ugenini, makosa madogo madogo niliyoyabaini katika mchezo uliopita, ninaendelea kuyafanyia kazi kwa lengo la kufanya vizuri zaidi," alisema Malale.

Kwa upande wa msemaji wa timu hiyo, Frank Lukwaro, alisema malengo yao ni kuhakikisha wanavuna pointi tatu katika mchezo huo.

"Tumeamua kuja mapema kwa ajili ya kuzoea mazingira pamoja na hali ya hewa, vilevile tunashukuru kwa mapokezi tuliyopewa," alisema Frank.

Mbeya City ambayo hivi karibuni iliachana na Kocha wao Mkuu, Amri Said, ipo nafasi ya pili kutoka mkiani ikiwa na pointi sita zilizotokana na kushinda mechi moja na sare tatu katika michezo tisa waliyocheza hadi sasa.

**KATUSUA...**




Mmoja kati ya washindi wa bonasi ya Jackpot ya SportPesa kwa mwezi Oktoba, Patrick Metusela, akionyesha mfano wa hundi ya Sh. milioni 25.8, baada ya kubashiri kwa usahihi mechi za Jackpot zinazochezwa kila wiki. **PICHA: SPORTPESA**

# Itaba ambadili Mbabe kuzipiga na Mkongo

**Na Mwandishi Wetu**

BONDIA maarufu nchini, Abdallah Pazy "Dulla Mbabe" ameondolewa kuzipiga na bondia kutoka DR Congo Alex Kabangu na nafasi yake imechukuliwa na Hussein Itaba, imeelezwa.

Pambano hilo limepangwa kufanyika Novemba 13, mwaka huu kwenye Ukumbi wa Next Door Arena, Oysterbay jijini Dar es Salaam ambapo siku hiyo pia bondia nyota nchini Hassan Mwakinyo atapigana na Jose Carlos Paz kutoka Argentina akiwania mikanda miwili.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Jackson Sport, Kelvin Twissa, alimwambia mwandishi wetu jana kuwa, mabadiliko hayo ni kawaida kutokea katika masuala ya ngumi za kulipwa, hivyo bondia huyo (Itaba) ameanza mazoezi kwa ajili ya kupambana na Kabangu.

Hivi karibuni Mbabe alipigwa kwa pointi dhidi ya bondia Bek Nurmaganbet mjini Atyrau, Kazakhstan. Bondia huyo alikwenda kupigana chini ya Promota Jay Msangi.

"Tumeona tufanye mabadiliko katika moja ya pambano letu kwa lengo la kupanua wigo na kujenga heshima katika ngumi za kulipwa nchini, hivyo mabadiliko hayo yamefanywa ili kupanua wigo wa mabondia na kuinua vipaji zaidi hapa nchini, naamini Itaba atafanya vema katika pambano hilo," alisema Twissa.

Alisema maandalizi ya mapambano ya 'Dar Fight Night' yanaendelea vizuri huku bondia bingwa wa mabara wa uzito wa Super welter, Hassan Mwakinyo, akijifua vikali. Mbali ya kutetea mkanda huo, Mwakinyo pia atawania ubingwa wa mabara wa uzito huo huo wa Chama cha IBA.

Mabondia kutoka nchi tano watazichapa kumsindikiza Mwakinyo na Paz, akiwamo aliyekuwa bingwa wa dunia wa WBC, Fatuma Zarika kutoka Kenya ambaye atazichapa na Patience Mastara wa Zimbabwe, na Zulfa Yusuph Macho atacheza na Alice Mbewe wa Zimbabwe.

Alisema kuwa wameamua kuingia kwenye mchezo wa ngumi kutokana na kutambua vipaji vya mabondia mbalimbali hasa Mwakinyo ambaye anafanya vizuri katika mapambano yake.

"Siku hiyo kutakuwa na mapambano makubwa ambapo mabondia kutoka nchi sita, Argentina, DR Congo, Kenya, Zimbabwe na wenyeji Tanzania watapigana, ni siku ambayo mashabiki wa ngumi za kulipwa wataona kitu tofauti kabisa katika mchezo huo, " alisema Twisa.

Alisema kampuni yao chini ya udhamini wa Azam TV, Hoteli ya Colosseum Dar es Salaam na Asas inauzoefu mkubwa katika kuandaa matamasha, masoko na shughuli mbalimbali na kuahidi kufanya jambo la kihistoria hapa nchini.

## Jackpot SportPesa yafika milioni 272. 8/-

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI ndiyo kwanza mwanzoni mwa Novemba, tayari dau la Jackpot ya SportPesa limefikia Sh. 272, 803,160, huku bonasi zikiendelea kumiminika kwa waliobashiri kwa usahihi kuanzia mechi 10-12 kwa Oktoba, mwaka huu.

Kampuni ya Kubashiri Matokeo ya SportPesa Tanzania, imeendelea kuongeza dau lao la Jackpot na kuwatangaza washindi wote wa Oktoba waliobashiri kwa usahihi kuanzia mechi 10-12.

Akifafanua zaidi Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas, amesema wanaendelea kutoa washindi kila wiki na kwa wiki iliyopita washindi kadhaa walifanikiwa kubashiri kwa usahihi mechi 10 mpaka 11."

"Tunahakikisha baada ya kukamilika kwa michezo yote ya mpira wa miguu, pesa inawekwa kwenye akaunti ya mshindi na kuwatangaza mara moja.

"Pia tunautaratibu wa kuwapigia simu washindi wetu wa bonasi ili kuwafahamisha zaidi juu ya ushindi wao na namna ya kutoa/kuhamisha fedha zao.

"Kitengo chetu cha huduma kwa wateja kinaendelea kufanya kazi kwa saa 24 kuhakikisha tunamhudumia mteja wetu haraka zaidi," Tarimba alisema na kuongeza.

"Kila wiki kama Jackpot ya SportPesa haijapata mshindi tunaongeza dau, lengo likiwa ni kuhamasisha na kuwaongezea wateja wetu nafasi ya kushinda zaidi."

## Waamuzi 45 Z'bar kufanya Copa Test

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

JUMLA ya waamuzi 45 wanatarajiwa kufanya mtihani wa utimamu wa mwili (Copa Fitness Test) kujiandaa na Ligi Kuu Zanzibar inayotarajiwa kuanza Novemba 14, huku mchezo wa Ngao ya Jamii ukitarajiwa kupigwa Novemba 8, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili Katibu wa Kamati ya Waamuzi Zanzibar, Muhsini Ali Kamara, alisema mtihani huo unatarajiwa kufanyika Novemba 6, mwaka huu katika Uwanja wa Amaan visiwani hapa.

Alisema Novemba 5, waamuzi wote wanaoshiriki mtihani huo watapimwa afya zao, ili kuhakikisha wanafanya Copa Test kwa kulingana na vipimo vya daktari atakayefanya zoezi hilo la upimaji.

Kamara alisema kwa upande wa waamuzi waliopo Kisiwani Pemba, watafanyia mtihani huo kisiwani humo, ambapo utasimamiwa na wakufunzi wa ndani wakiongozwa na Kamishna Ali Juma Sallim.

"Tumechelewa kufanya Copa Test hii kulingana na ligi msimu uliopita kuchelewa kumalizaka, lakini hata msimu huu nchi ilikuwa katika uchaguzi na kiwanja ambacho kinatumika kufanya mtihani huo kilikuwa na shughuli za kiserikali," alisema.

Michezo
Jumatano Novemba 4, 2020
Nipashe



GUARDIOLA AIKATAA MAZIMA BARCELONA HABARI UK 22

KUCHEKA TENA LEO?...



Pascal Wawa (kulia), akishangilia na wachezaji wenzake wa Simba baada ya kuifungia timu yake kwenye mechi dhidi ya Gwambia FC iliyopigwa Uwanja wa Mkapa hivi karibuni na kushinda kwa mabao 3-0. Mashabiki wa timu hiyo wanatarajia furaha kama hiyo leo watakapoikaribisha Kagera Sugar katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam. **PICHA: MAKTABA**

# YANGA YAJITULIZA KILELENI LIGI KUU

Nyuki wasimamisha mechi Gwambina ikiwakwamisha Misungwi, lakini yaishusha Azam...

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kushinda mechi saba mfululizo, hatimaye timu ya Yanga jana ilikwaa kisiki kwa kulazimishwa sare ya bila kufungana na Gwambina FC kwenye Uwanja wa Gwambina, Misungwi nje kidogo ya Jiji la Mwanza, lakini matokeo hayo hayakuizuia kukaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Bara.

Hii inakuwa mara ya kwanza kwa Yanga kucheza mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu na kumaliza dakika 90 bila kufunga bao.

Yanga ambayo hiyo ni mechi ya mwisho kabla ya kucheza na watani wao wa jadi, Simba Jumamosi, haikuwa bora kipindi cha kwanza, badala yake ilicharuka kipindi cha pili, lakini haikuwa makini katika umaliziaji, huku kipa wa Gwambina, Ibrahim Isihaka, akiwa kikwanzo kikubwa kwao.

Kipindi cha kwanza Gwambina alianza kukaa nyuma ya mpira na kuwaachia Yanga kucheza pasi fupi fupi, lakini wapinzani wao walionekana kutoelewana kutokana na mfumo waliocheza.

Shambulizi la kwanza kwa Gwambina lilikuwa dakika ya 16, wakati Rajab Athumani alipopiga faulo iliyookolewa kwa ustadi na kipa Metacha Mnata na kuwa kona ambayo haikuwa na hatari yoyote kwenye lango la Yanga.

Dakika ya 23, straika mkongwe, Jacob Massawe akiwa nje ya eneo la hatari, alichia shuti kali lililotemwa na kipa Metacha, lakini wachezaji wa Gwambina walikuwa mbali na kukosa mmaliziaji, huku mabeki wa Yanga wakiuwahi na kuuokoa.

Yanga ilianza kufanya shambulizi la maana langoni mwa Gwambina kwenye dakika ya 29, Tuisila Kisinda alipoupata mpira uliokosewa na beki mmoja wa timu hiyo, akiwa peke yake yeye na kipa Ibrahim alipiga shuti dhaifu lililoishia mikononi mwa kipa.

Sekunde chache tu baada ya kuanza kipindi cha pili, nyuki walivamia uwanja na kusababisha wachezaji, waamuzi, makocha na baadhi ya mashabiki kulala chini ili kujinusuru.

Mechi iliendelea baada ya kuonekana kuna usalama na iliwachukua Gwambina dakika tano kufanya shambulizi kali, lakini shuti la Revocatus Richard lilipanguliwa na kipa Metacha na kuwa kona tasa.

Kutoka kwa Waziri Junior na kuingia kwa Michael Sarpong kulionekana kuipa uhai Yanga na kuanza kufanya mashambulizi mfululizo kwenye lango la wapinzani wao, dakika ya 58, alipopiga shuti kali lililotoka nje kidogo ya lango, lakini dakika moja baadaye straika huyo alipiga shuti lingine akiwa kwenye eneo la hatari likapanguliwa na kipa Ibrahim.

Nusura Yanga iandike bao dakika ya 65, baada ya krosi safi ya Deus Kaseke kumkuta Yacouba Songne ambaye aliupiga kichwa na kuonekana kuzama wavuni, lakini ulimgonga mguuni beki mmoja wa Gwambina na mpira ukasimama karibu na lango kabla ya kipa kuuchupia na kuiweka timu yake salama.

Kwa matokeo hayo, Yanga sasa inaongoza ligi hiyo ikiwa imekusanya pointi 23, moja zaidi ya Azam FC iliyokuwa ikiongoza kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa huku ikiwa mchezo mmoja mbele, lakini sasa timu hizo kila moja imecheza mechi tisa. Kwa upande wa Gwambina inafikisha pointi 10 kwa mechi 10 ambazo imecheza mpaka sasa ambazo zinaifanya kushika nafasi ya 12.

## WAAMUZI SIMBA, YANGA WAONYWA

**Na Adam Fungamwango**

MWENYEKITI wa Kamati ya Waamuzi, Sudi Abdi, amewataka waamuzi watakaochezesha mechi ya watani wa jadi, Simba na Yanga Jumamosi kuwa makini na kufuata sheria zote 17 za soka, kutokana na uzito wa mchezo huo pamoja na presha iliyopo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Sudi, mwamuzi wa zamani wa kimataifa nchini, alisema mechi ya Simba na Yanga huwa inavuta hisia za watu wengi na inakuwa na maneno mengi, hivyo waamuzi wanatakiwa kuwa makini kwenye uchezeshaji, kwani makosa hata machache watakayofanya yanaweza kusababisha taswira mbaya.

**"Kwa sasa soka letu linaangaliwa sana hata nje, na pia mechi hii itaangalia na watu wengi, hivyo waamuzi wanapaswa kuwa makini hasa kwenda sawa na matukio uwanjani, pamoja na kuwa na utimamu wa mwili," alisema.**

Sudi alisema mchakato wa kuchuja waamuzi na kuwapata wale watakaochezesha mechi hiyo umekamilika na wanaweza kutangazwa kwa muda uliopangwa.

Yanga inatarajiwa kuikaribisha Simba kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, hiyo ikiwa ni mechi ya kiporo ya Ligi Kuu Tanzania Bara raundi ya sita.

Hii itakuwa ni mara ya kwanza kwa timu hizo kukutana msimu huu, lakini ambapo mara ya mwisho zilikutana kwenye hatua ya nusu fainali ya Kombe la FA katika Uwanja wa Benjamin Mkapa na Simba kuondoka uwanjani na ushindi wa mabao 4-0.

Kwenye mechi ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara Januari 4, mwaka huu, timu hizo zilitoka sare kwa kufungana mabao 2-2 na mechi ya mzunguko wa pili, Yanga iliichapa Simba bao 1-0, mechi ikichezwa Machi 8, mwaka huu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002